

**TUIMARISHE KISWAHILI
CHETU: KITABU CHA
WANAFUNZI WA
MWAKA WA PILI/TATU**

**BUILDING PROFICIENCY IN
KISWAHILI: A MANUAL FOR
SECOND/THIRD YEAR
SWAHILI STUDENTS**

LIOBA J. MOSHI

**TUIMARISHE KISWAHILI CHETU:
KITABU CHA WANAFUNZI WA
MWAKA WA PILI/TATU**

*Building Proficiency in Kiswahili:
A Manual for Second/Third Year
Swahili Students*

Lioba J. Moshi

**University Press of America,[®] Inc.
Lanham · Boulder · New York · Toronto · Plymouth, UK**

**Copyright © 1988 by
University Press of America,® Inc.
4501 Forbes Boulevard
Suite 200
Lanham, Maryland 20706
UPA Acquisitions Department (301) 459-3366**

**Estover Road
Plymouth PL6 7PY
United Kingdom**

**All rights reserved
Printed in the United States of America
British Library Cataloging in Publication Information Available**

Illustrated by Susan Harby

Library of Congress Cataloging-in-Publication Data

Moshi, Lioba J.

**Tuimarisho Kiswahili chetu : kitabu cha wanafunzi wa mwaka
wa pili/tatu = Building proficiency in Kiswahili : a manual for
second/third year Swahili students / Lioba J. Moshi.**


p. cm.

Bibliography: p.

- 1. Swahili language—Text-books for foreign speakers—English.
I. Title. II. Title: Building proficiency in Kiswahili.
PL8702.M67 1988
496'.39282421—dc19 87-27466 CIP**

ISBN-13: 978-0-7618-3550-9 (paperback : alk. paper)

ISBN-10: 0-7618-3550-4 (paperback : alk. paper)

 **The paper used in this publication meets the minimum
requirements of American National Standard for Information
Sciences—Permanence of Paper for Printed Library Materials,
ANSI Z39.48—1984**

Kwa wanafunzi wangu wote, ndugu na marafiki.
“Penye nia pana njia.”



Shukrani

Ningependa kutoa shukrani za dhati kwa watu wote walioshiriki katika kuifanikisha kazi hii. Hasa ningependa kuwashukuru wakuu wa sehemu ya *Masomo ya Kiafrika ya Chuo Kikuu cha Stanford na Chuo Kikuu cha California, Berkeley*, Profesa James Lowell Gibbs, Jr. (Stanford) na Profesa David Leonard (Berkeley) kwa ruzuku iliyoniwezesha kuifanya na kuikamilisha kazi hii. Ningependa kumshukuru Bibi Susan Harby kwa kujitolea kwa masaa mengi kuchora picha zilizomo katika makala haya. Bila shaka picha hizi zimeimarisha umuhimu wa utamaduni na mila za Mwafrika. Ningependa pia kuwashukuru wanafunzi wa Kiswahili wa vyuo vikuu vya Stanford na Berkeley kwa kutumia nakala ya awali ya makala haya. Shukrani zangu za dhati zimwendee Ladislaus J. Semali ambaye amenipa moyo wa kuendelea na kazi hii hadi imemalizika, na pia kwa kuhakiki makala hii. Maoni yake juu ya sehemu mbalimbali za makala hii yalikuwa msaada usio na kifani. Pia ninapenda kumshukuru Elizabeth J. Frazer kwa kazi kubwa ya kusahihisha baadhi ya sehemu za makala hii. Shukrani nyingi ziwaandee: Profesa Abdulaziz Abdalah wa Chuo Kikuu cha Nairobi, Bibi Albina Chuwa, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa mawazo yao ambayo yalinipa mwangaza juu ya mambo yafaayo kutumiwa katika makala hii kuridhisha kiwango kilichokusudiwa.

Lioba Moshi

Yaliyomo

Shukrani iii

Utangulizi iv

Somo la Kwanza 1

Mazoezi maalum: A na B 1

Ufahamu: Mazungumzo 2

Maswali ya Ufahamu 3

Kazi Maalum 3

Habari za Sarufi 3

'a'of association 3

Contractions 4

Reduplication 5

The Possessive forms 6

Other possessive forms 6

Msamiati 7

Somo la Pili 9

Mazoezi maalum: A, B na C 10

Ufahamu: Ujamaa Vijijini 10

Maswali ya Ufahamu 10

Kazi maalum 10

Habari za Sarufi 11

ote, o ote 11

Msamiati 12

Somo la Tatu 13

Mazoezi maalum: A na B 13

Ufahamu: Maisha ya Nyumbani 15

Maswali ya Ufahamu 16

Kazi maalum 16

Habari za sarufi 16

Irregularity in noun classes 16

Diminutives 17

Augmentatives 18

Collectives	19
Msamiati	19
Somo la Nne	21
Mazoezi Maalum: A, na C	21
Malezi ya Watoto	21
Maswali ya Ufahamu	22
Kazi maalum	22
Habari za sarufi	23
The Relative form	23
The negative of a relative form	23
Msamiati	24
Somo la Tano	25
Mazoezi maalum: A na B	25
Usafiri Unguja	25
Maswali ya Ufahamu	25
Kazi maalum	27
Habari za sarufi	27
The Passive form	27
Msamiati	29
Somo la Sita	31
Mazoezi maalum: A na B	31
Sehemu za Mwili	32&33
Matumizi ya Lugha	34
Maswali ya Ufahamu	34
Kazi maalum	35
Habari za sarufi	35
More on Relativization	35
Msamiati	36
Somo la Saba	37
Mazoezi maalum: A na B	37
Ufahamu: Uhuru ni Nini?	37
Maswali ya Ufahamu	38
Kazi maalum	39
Habari za sarufi	39
The infinitive form	39
Msamiati	42
Somo la Nane	45
Mazoezi maalum: A, B na C	45

Mashairi	46
Shairi juu ya Mkulima	46
Maswali ya Ufahamu	47
Kazi maalum	48
Msamiati	48
Somo la Tisa	49
Mazoezi maalum: A, B na C	49
Adui wa Wakulima	50
Maswali ya Ufahamu	51
Kazi maalum	52
Habari za Sarufi	52
The -ka- aspect marker	52
The negative of -ka-	52
Msamiati	53
Somo la Kumi	55
Mazoezi maalum: A na B	55
Adui wa Afya	56
Maswali ya Ufahamu	57
Kazi maalum	58
Habari za Sarufi	58
More on negatives	58
Msamiati	60
Soma la Kumi na Moja	61
Mazoezi maalum: A na B	61
Mchezo wa Ng'ombe	61
Maswali ya Ufahamu	63
Kazi maalum	63
Habari za sarufi	63
Conditional tenses	63
Msamiati	67
Somo la Kumi na Mbili	69
Mazoezi maalum: A na B	69
Michezo Shuleni	70
Maswali ya Ufahamu	70
Kazi Maalum	70
Habari za sarufi	70
The causative form	70
Msamiati	73

Somo la kumi na Tatu 75

- Mazoezi maalum: A, B na C 75
- Ufahamu: Ukosefu wa Maji Vijijini 76
- Maswali ya Ufahamu 76
- Kazi maalum 77
- Habari za sarufi 77
- The Stative form 77
- Msamiati 79

Somo la Kumi na Nne 81

- Mazoezi maalum: A, B na C 81
- Ufahamu: Muundo wa Mashairi 83
- Shairi la 'Kipi Bora' 83
- Maswali ya Ufahamu 83
- Shairi la 'Mapatano' 84
- Maswali ya Ufahamu 84
- Kazi maalum 85
- Msamiati 86

Somo la Kumi na Tano 87

- Mazoezi maalum: A na B 87
- Ufahamu: Huduma za Afya Kisiwani Unguja 88
- Maswali ya Ufahamu 89
- Kazi maalum 89
- Habari za sarufi 90
- Conjunctions 90
- Msamiati 91

Somo la Kumi na Sita 93

- Mazoezi maalum: A, B na C 93
- Ufahamu: Ajali Haina Kinga 94
- Maswali ya Ufahamu 95
- Kazi maalum 95
- Habari za sarufi 95
- Interjections 95
- Msamiati 97

Somo la Kumi na Saba 99

- Mazoezi maalum: A na B 99
- Ufahamu: Elimu ya Kujitegemea 100
- Maswali ya Ufahamu 101
- Kazi maalum 101

Msamiati	102
Somo la Kumi na Nane	103
Mazoezi maalum: A na B	103
Ufahamu: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	103
Maswali ya Ufahamu	105
Kazi maalum	106
Habari za sarufi	106
Usemi wa msemaji ('direct speech')	106
Fractions	106
Msamiati	107
Somo la Kumi na Tisa	109
Mazoezi maalum: A na B	109
Ufahamu: Kuchagua Mchumba kwa Wachaga	109
Maswali ya Ufahamu	110
Kazi maalum	111
Habari za sarufi	111
Auxiliary verbs	111
Msamiati	113
Somo la Ishirini	115
Mazoezi maalum: A na B	115
Ufahamu: Uteuzi wa Lugha ya Taifa	116
Maswali ya Ufahamu	117
Kazi maalum	118
Msamiati	119
Nyongeza	121
Methali	121
Vitendawili	125
Majibu ya Vitendawili	126
Misemo	126
Majibu ya Maswali katika Masomo	129
Jedwali	143
Msamiati	145
Maelezo (footnotes)	163
Marejeo ya Vitabu	

INTRODUCTION

1. About the Manual

"Tuimarisha Kiswahili Chetu" is a manual intended for students who have had at least a year of Kiswahili or the equivalent.

The manual is primarily intended for classroom use. It may, however, be used by individual students outside of the classroom. It will be more useful in a classroom situation where the instructor's help is available and where contact with other students is possible in order to improve conversational skills. The materials in the manual are intended to help the student to steadily build proficiency in the language by speaking, reading to understand, and writing. Consequently, there is an emphasis on conversation, comprehension and composition while strengthening those parts of the grammar that are essential in mastering the language. Each lesson contains a section on special exercises (**Mazoezi Maalum**), a passage for comprehension (**Ufahamu**), questions from the comprehension passage (**Mazoezi ya Ufahamu**), special assignment (**Kazi Maalum**), a brief description of selected parts of the grammar (**Habari za sarufi**), and vocabulary from the exercises and the comprehension passage (**Msamiati**).

2. Mazoezi Maalum

These are exercises emphasizing a specific aspect of the grammar. Answers to these exercises can be found in the appendix **Nyongeza** at the end of the manual. It is recommended that the parts of grammar involved in these exercises are reviewed before the students attempt to do the exercises. Alternatively, the instructor can assign the exercises in advance to determine the level of difficulty and consequently how much of the grammar in that lesson need to be reviewed.

3. Ufahamu

The passages in this section provide a wide range of subjects that can be used as a stimulus for further discussions in class or as the basis for essay writing. The passages are selected in such a way that the student is able to build on what he/she already knows from the previous exercises. If the manual is used systematically, the student will notice satisfying progress in his/her competence and performance in the language.

4. Maswali ya Ufahamu

These are a set of comprehension questions and exercises intended to improve the student's comprehension skills as well as make use of the vocabulary used in the reading. Students should be encouraged to use their own words as much as possible rather than copying the answers straight from the passage. Some of the questions demand a thorough understanding of the passage in order to give an appropriate answer. That is, some of the questions require some creativity and the ability to relate the information in the passage with personal and everyday experiences.

5. Kazi Maalum

Kazi Maalum is an exercise that can be used for essay writing or class discussion. It draws from the comprehension passage. It is designed to stimulate a fruitful class discussion. It is also an opportunity for the students to put to practice the new vocabulary and grammar. If it is used as an essay assignment, it is a good idea for the students to read their essays in class. This will be a chance for the students to share their ideas using the language. Other students should be encouraged to ask questions arising from the student's essay. Thus the class will have an opportunity to work together more. A language is best learned in context rather than in isolation. Student participation helps the learner to develop personal confidence in using the language. **Kazi Maalum** can also be used instead of a regular test or examination.

6. Habari za Sarufi

The grammar section provides a summary of specific points of grammar in that lesson. The manual is not intended to serve as a Swahili grammar book. There are ample grammar books on the market that can be used to supplement what the grammar section at the end of each lesson provides. The ultimate aim is to improve the student's communicational skills rather than his/her competence in Swahili grammar.

7. Msamiati

At the end of each lesson there is a vocabulary list mainly from the **Mazoezi Maalum** and **Ufahamu**. In addition, there is a master list at the end of the manual for quick reference. If a word is preceded by a dash (-) it indicates that word is a verb. When there is no dash it is a noun, adjective or an adverb. The vocabulary list is by no means exhaustive. It is advisable for students to own a Swahili-English Dictionary. However, the students are encouraged to focus on the context in which a word is used for its contextual meaning. Using the vocabulary in sentence building and essay writing is also strongly recommended.

8. Appendices

The Appendix has five parts. Part one, which is **Methali**, contains the most commonly used 'Proverbs'. Part two contains the most commonly used **Vitendawili** 'Riddles'. Part three, which is **Misemo**, contains the commonly used 'Sayings'. An English translation is provided for each 'Proverb', 'Riddle', and 'Saying'. The 'Proverbs' and 'Sayings' can be used as a basis for essay and story writing. They can also be used as a basis for discussions in the class where students talk about how they understand a particular 'Proverb', or 'Saying'. At best, 'Riddles', can be used just for fun.

Part four contains answers to the exercises at the beginning of each lesson (i.e. **Mazoezi Maalum**). Part five, which is **Jedwali**, contains a summary of essential pronominal concord for quick reference.

SOMO LA KWANZA

MAZOEZI MAALUM

A. Jaza nafasi hizi kwa kutumia 'a' ya uhusiano ("preposition")

1. Mwanafunzi kwanza.
2. Mambo shule.
3. kabla kulala.
4. Nyuzikushonea.
5. Somo Kiswahili.
6. Visanduku barua.
7. Uhuru nchi Afrika.
8. Sura watu hawa.
9. Nyumbani wazee wangu.
10. Nafasikusoma.

B. Jaza nafasi zilizoachwa kwa kutumia 'a' ya uhusiano

1. Wafanyakazi walikuwa furaha kwa sababu ilikuwa siku ya kupumzika.
2. Wanafunzi watakuwa na siku mbili kupumzika kesho.
3. Walipewa nafasi kuzungumza na wageni.
4. Kuna mashindano mbalimbali, kama vile, mpira kikapu, mbio masafa marefu, mbiokupokezana, na mashindano ndondi.
5. Wanafunzi wanapenda mashindano mchezo soka.
6. Hawana maji na chakula kutosha.
7. Watawapa pesa na mahitaji mengine safari.

C. Tumia "ake" na kamilisha vifungu hivi

- | | |
|------------------|-----------------|
| 1. mama..... | 6. sikio..... |
| 2. mto..... | 7. ng'ombe..... |
| 3. kikapu..... | 8. rafiki..... |
| 4. nywele..... | 9. maziwa |
| 5. nyumbani..... | 10. ukuu..... |

- Aisha..... Hujambo kaka, jina langu ni Aisha
- Ayubu..... Sijambo dada Aisha. Jina langu Ayubu
- Aisha..... Ninafurahi kukufahamu. Unatoka wapi Ayubu?
- Ayubu..... Natoka Kenya, sehemu za Afrika ya Mashariki. Na wewe je?
- Aisha..... Natoka sehemu hizo hizo, lakini si Mombasa.
- Ayubu..... Bado ninasubiri Aisha, au hutaki kuniambia watoka wapi.
- Aisha..... Unaweza kubuni. Jaribu mara tatu kama hutaweza kubuni nitakuambia.
- Ayubu..... Aaa...mmm... Nafikiri unatoka Kenya pia labda Nairobi.
- Aisha..... Hapana Ayubu, nitakusaidia kidogo. Sitoki Kenya. Kwa hivyo Naitoka si mji wangu.
- Ayubu..... Sasa nimefahamu. Unatoka Tanzania sivyo ?
- Aisha..... Ndio, lakini Tanzania ni kubwa. Bado hujabuni mji wangu.
- Ayubu..... Aisha, hii si haki. Mimi nilikuambia jina langu na ninatoka wapi lakini wewe unanipa kazi ya kubuni unatoka wapi. Hii si haki hata kidogo.
- Aisha..... Haya basi. Kwa kweli nilizaliwa Unguja lakini sasa wazazi wangu wamekuja Tanzania Bara, mjini Tanga.
- Ayubu..... Ahaa. Unafanya nini hapa Marikani?
- Aisha..... Ninasoma. Ninasoma Chuo Kikuu cha Stanford. Na wewe, unafanya nini hapa?
- Ayubu..... Ninatembea tu. Wazazi wangu ni wafanyi biashara. Wana duka la ng'ani huko nyumbani. Sasa wamekuja hapa kwa shughuli za biashara yangu. Mimi nimekuja nao ili nione Marikani kidogo.
- Aisha..... Hii ni mara yako ya kwanza kufika Marikani?
- Ayubu..... Ndio, lakini nimetembea sana Ulaya, hasa Uingereza, Ujerumani, Ufaransa. Nilisoma Uingereza katika Chuo Kikuu cha Oxford.
- Aisha..... Ulisomea nini?
- Ayubu..... Nilisomea mambo ya biashara. Ninategemea kuwasaidia wazazi wangu wanao na labda baadaye nitaanza biashara yangu mwenyewe.
- Aisha..... Ni mawazo mazuri hayo. Labda tutaonana tena. Ni lazima niondoka sasa. Rafiki yangu ananisubiri.
- Ayubu..... Asante. Mimi pia, nimefurahi kuzungumza nawe. Nitafurahi kukufurahi tena. Labda unaweza kunipigia simu leo jioni.
- Aisha..... Aaa.....mmmm....
- Ayubu..... Simu yangu ni mbili- mbili- nne, sifuri- moja- sita -tatu., au takupigia mimi. Simu yako ni.....?
- Aisha..... Haidhuru, nitakupigia mimi. Kwa heri Ayubu.
- Ayubu..... Kwa heri ya kuonana Aisha.

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu maswali yafuatayo

1. Mazungumzo haya ni kati ya nani?
2. Aisha na Ayubu ni marafiki?
3. Toa sababu kwa jibu lako la 2.
4. Aisha na Ayubu wanatoka nchi moja?
5. Aisha na Ayubu wako Marikani lakini kila mmoja ana sababu tofauti za kuwa Marikani. Taja sababu hizo.
6. Kwa nini Ayubu alisema: "Hii si haki hata kidogo?"

Andika sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo ili kuleta maana kamili

-subiri	buni	si haki
bara	wafanyi biashara	shughuli
-taja	maana kamili	

Kazi Maalum

Wanafunzi waandae mazungumzo baina ya watu wawili au zaidi. Mazungumzo haya yanaweza kutumiwa darasani kwa njia ya mchezo wa kuigiza.

HABARI ZA SARUFI

A. The 'a' of association

This form was referred to in the exercises as **-a ya uhusiano**. It is also known as **'a' binder**.

In the example: *somo la Kiswahili*, the **a** of **la** associates or binds *somo* to *Kiswahili*. The prefix of the binder is the class-designator of the subject. That is, the same prefix that appears on verbs to designate the subject of that verb.

With the pronoun concord, **a** makes the phrase an adjective with

- (a) A possessive concept.

For example:

mtoto wa Juma.

- (b) A descriptive concept.

For example:

mtoto wa tatu.

kiti cha mbao.
mahali pa kupendeza.

With **ku**, **-a** helps to express an adverbial concept.

- (a) By means of.
For example:
kwa motokaa.
- (b) By reason of.
For example:
kwa hasira.
- (c) Manner or state.
For example:
kwa bidii.
- (d) Place.
For example:
kwa Mzee Juma. 'at mzee Juma's (place).
- (e) In respect to.
For example:
Wote walikaribishwa, wazee kwa watoto.
"All were invited, old and young"

With '**n**' of **association**, it may be interpreted as a preposition or a conjunction.

- (a) Prepositional.
For example:
Alikwenda na Juma. "He went with Juma."
Alikuwa nacho. "He was with it/He had it."
Ninaye kaka mmoja. "I am with/I have one brother."
- (b) Conjunctional.
For example:
mama na mwanaye. "A mother and her child."

B. Contractions

Sometimes when **na** with the conjunctional concept is used with a personal pronoun, we may get a contracted form as in **nao** which is a contracted form of **na + wao**. Thus,

na + mimi → nami

na + wewe → nawe
na + yeye → naye
na + sisi → nasi
na + ninyi → nanyi
na + wao → nao

Note the following when associating **-a** with the following class-designators.

1. In class 1, the **wa** is derived from **yu**. This is the same **yu** that you find in **yule** "that one". Thus, **yu + -a → yua → ywa → wa**. The plural which is what we are calling class 2, is **wa**. Thus, **wa + a → wa**.
2. In class 3, **u + a → wa**. The plural, class 4, **i + a → ya**. The same applies to class 6, the plural of class 5.
3. In class 7, **ki + a → cha**. Its plural, class 8, **vi + a → vya**.
(see "Jedwali" pg. 130 for the noun class and agreement system chart).

C. Reduplications

Reduplication intensify as well as make anaphoric reference to something that has just been said. We saw one kind of reduplication in the Reading Lesson **hizo hizo**. These are called emphatic demonstrative forms or intensifiers. When any of these forms is used it has to agree in class with the element to which it is making anaphoric reference. In the Reading Lesson, *Ayubu* says: "Natoka Kenya, Afrika ya Mashariki." *Aisha* says: **Natoka sehemu hizo hizo**. **Hizo hizo** implies **Afrika ya Mashariki** which is what *Ayubu* just said. Here is a short dialogue with some more examples of reduplication.

M: Unakwenda wapi Aisha?

A: Ninakwenda Montreal, na wewe je?

M: Ninakwenda huko huko.

A: Aa... ni ajabu sivyo, kuwa tuna safari moja. Unakwenda kufanya nini huko Montreal?

M: Kuna mkutano wa masomo ya Kiafrika.

A: Vizuri. Na mimi ninakwenda kwenye mkutano huo huo.

M: Unachukua ndege gani?

A: American Airways. Na wewe je?

M: Hiyo hiyo.

In the dialogue I have used only a few of the intensifiers. Any demonstrative can be used similarly to satisfy the needed emphasis (cf. Ashton (1947, p. 305-307) for additional discussion on contractions).

D. The Possessive form

The basic ones are: **-angu, -ako, -ake, -etu, -enu, -ao**. Like the **a** of association, they take a class designator of the subject. However, there are some irregularities with nouns of kinship. For example, **baba, mama, babu** and others referring to animals like **ng'ombe, paka, simba**. Because such nouns do not show a distinction between singular /plural (For example, **mtoto, watoto**) they are included in class 9/10 (generally known as the **n/n** or **ø/ø** class). Nevertheless, they do not exclusively follow the agreement patterns of nouns under this group. Except in association with possessive forms and the **a** of association, these nouns follow the pattern used by nouns in the **m /wa** group otherwise called class 1/2.

While speakers may say:

babu wa/ya Juma, babu wa/za Juma,
they would say:

babu yangu, babu zangu (but not **babu wangu**).

With non-human nouns, speakers may say:

singular: **ng'ombe wa Juma** (and not **ng'ombe ya Juma**)

Plural: **ng'ombe wa /za Juma**

Singular: **ng'ombe wangu** (and not **ng'ombe yangu**)

Plural: **ng'ombe wangu/zangu**.

E. Other Possessive forms

-enye denotes "having" something or an activity. Its object must always be expressed. For example,

mwenye nyumba where **nyumba** is the possessed object. **-enye** takes the class designator of the subject just like the other possessive forms discussed above except when referring to a living being. In such a case, it takes the noun concord. For example:

duka lenye vitabu - "a shop with books."

but:

mtu mwenye chakula - "a person with food."

Ng'ombe mwenye shingo ndefu - "A cow with a long neck."

The form **-enyewe** is used with any noun for emphasis and translates to "alone", "precisely", "the one in reference". It stresses the identity of that noun. For agreement, it follows the same rules as **-enye**. Thus:

mzee mwenyewe alikuwa na pesa nyingi.

"The oldman himself had a lot of money."

kitabu chenyewe kina picha za wanyama.

"The book itself has pictures of animals."

Note: Both of these examples have been given the neutral interpretation. If **-enyewe** is stressed, the interpretation will include 'precisely'. If the nominal (That is, **mzee**, **kitabu**) is stressed, the interpretation will imply 'the one in reference'.

MSAMIATI

-buni	guess.
haidhuru	never mind, no harm, harmless.
haki	fairness, right, justice, lawfulness.
mbio za kupokezana	relay race.
mbio za masafa marefu	marathon.
mpira wa kikapu	netball, basketball.
ndondi	boxing.
-pokea	receive.
-pokezana	act of giving and receiving from one another.
shughuli	business, engagement, occupation.
soka	soccer.
-subiri	wait, be patient.

SOMO LA PILI

MAZOEZI MAALUM

A. Tumia ‘-ote’ kwa kukamilisha vifungu hivi

- | | |
|--------------------|--------------------|
| 1. wakulima..... | 2. majemadari..... |
| 3. wakufunzi..... | 4. watalii..... |
| 5. kiangazi..... | 6. uhuru..... |
| 7. kutafakari..... | 8. nyumba..... |
| 9. magonjwa..... | 10. kisigino..... |
| 11. chura..... | 12. mizizi..... |

B. Tumia ‘-o -ote’ kwa kukamilisha vifungu hivi

- | | |
|----------------|-------------------|
| 1. mzee..... | 2. ukuta |
| 3. jicho..... | 4. kidole |
| 5. mlima..... | 6. mbwa |
| 7. mahali..... | 8. bibi..... |
| 9. shoka..... | 10. motokaa |

C. Jaza nafasi kwa kutumia vipengele vilivyowekewa alama ()

1. Nili.....ona jana (ku, ni).
2. Juzi nilikuwa hapa, nani ali.....ona (m, ni)?
3. Mwalimu amekuja hapa, tuli.....pa zoezi la nyumbani (ku, ni, m).
4. Wageni walikuwa hapa, tuli.....peleka kuona sinema (ku, ni, wa, mw).
5. Kama mgonjwa atakuja leo, daktari ata.....ona (ni, mw, wa).
6. Je, baba ali.....ambia nini mama (ni, ku, mw)?
7. Je, ali.....ambia nini sisi (ku, tu, wa)?
8. Je, wageni watafika lini? Ninataka ku.....ona (tu, wa, mw).
9. Ninataka ku.....ambia kitu wewe si wao (tu, wa, ku).
10. Ninajua kila kitu unachotaka ku.....ambia watu hawa (ku, m, wa).

Ufahamu

UJAMAA VIJIJINI¹

Jamaa ya Kiafrika ya zamani iliishi kwa misingi ambayo sasa tunaiita misingi ya ujamaa. Kama unawauliza wanaishije, hawatakujibu kisiasa kama tunavyojibu sasa kwamba wanaishi kijamaa. Waliishi tu kijamaa na wala hawakujua namna nyingine ya kuishi. Waliishi pamoja na kufanya kazi pamoja kwa sababu hivyo ndivyo walivyoelewa maisha. Hivyo ndivyo walivyo-weza kusaidiana kupambana na matatizo mbalimbali ya maisha - mvua na jua, maradhi, hatari za wanyama au binadamu wengine, na safari nzima ya tangu kuanza maisha mpaka kufikia mauti.

Matunda ya kufanya kazi pamoja hayakuwa yakigawanywa sawa sawa kabisa, lakini sheria za kugawanya zilijulikana na pia misingi yake ilikuwa kwamba kila mmoja wa jamaa ana haki ya kupata chakula cha kutosha, mavazi ya kutosha, na mahali pa kulala kabla mwingine (hata mkubwa wa jamaa) hajapata zaidi ya hapo. Walijiona kwamba ni kitu kimoja; na lugha yao na vitendo vyao vilisitiza umoja wa jamaa yao. Mahitaji ya lazima ya maisha yalikuwa ni “chakula chetu”, “ardhi yetu”, na “ng’ombe wetu”. Hata namna ya kuwasiliana ilisitiza umoja na uhusiano wa jamaa. Mzee Fulani, Mjomba Fulani, Shangazi Fulani, Binti Fulani au Bin Fulani; mama Fulani au Baba Fulani; au mke mwenzi Fulani na kadhhalika. Waliishi pamoja na kufanya kazi pamoja; na matunda ya kazi yao yalikuwa ni mali ya jamaa nzima.

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu maswali haya

1. Mwandishi wa habari hii anasema misingi ya ujamaa ni nini?
2. Jamaa ya kiafrika iliishije?
3. Matunda ya kazi ya pamoja yalikuwa mali ya nani? Yaligawanywa sawa sawa?
4. Kwa nini watu walikuwa na namna maalumu wa kuitana? Waliitanaje?

Tumia maneno haya katika sentensi

msingi	kupambana	gawanya
kujiona	sisitiza	uhusiano

Kazi maalum

Wanafunzi wafafanue mada ya “Ujamaa” waielewavyo. Wanaweza kujadiliana juu ya faida au hasara za kuishi kijamaa.

HABARI ZA SARUFI

ote and o ote

ote and **o ote** may be used with nouns to qualify or describe them. Some grammars call them adjectives. However, they have a quantifier and a qualifier function. The interpretation of **ote** depends on whether the noun in association is singular or plural. If it is singular, it implies “wholeness”, “completeness”. If it is plural, it implies “total”.

For example:

Mti wote - “the whole / entire tree.”

Miti yote - “all the trees.”

It may sound strange to native speakers if you say **mtu yote** although in English you can conceptualize “a whole person”. For native speakers of Kiswahili, a person is whole and is not made up of single pieces. A whole person is generally referred to as **mtu mzima** which also means “an adult” or “a healthy person.”

The interpretation of **o ote** is not affected by the singular / plural distinction of the noun. It may be translated to “any”, “whatsoever”, “whoever” etc... depending on the general interpretation of the noun.

For example:

mtu ye yote “anyone”, “whoever”.

mahali po pote “any place”, “anywhere”.

For Example:

Mtu ye yote anaweza kwenda kumwona rais wa nchi?

Kama wewe ni mgeni, unaweza kutembea mahali po pote?

MSAMIATI

-chota	take up water a little at a time.
chura	frog.
-elewa	understand, comprehend.
-fafanua	explain.
fulani	some fellow, so and so.
-ishi	live, survive, exist.
-jadili	discuss.
kiangazi	summer, hottest season of the year.
(ki)sigino	heel.
mada	notion.
(ma)jemadari	army general.
maradhi	disease in general, sickness.
(m)singi	foundation, primary.
mauti	death.
-pambana	confront, deal with severely.
shangazi	aunt
shoka	axe.
-sisitiza	insist, enforce.
tafakari	think.
uhusiano	relationship.
(vi)pengele	a part of (i.e a part of a word).
(wa)kufunzi	instructor.
-wasiliana	communicate with each other.
(wa)talii	tourist.

SOMO LA TATU

MAZOEZI MAALUM

A. Tumia '-a' ya uhusiano ili kukamilisha vifungu hivi

1. Mwanafunzi chuo kikuu Dar es Salaam.
2. Nyumba mzee Juma kijiji Mbezi.
3. Barua (wingi) washiriki michezo..... Olympiki.
4. Mlangoni meneja kiwanda kutengenezea viatu.
5. Kifo..... baba yake kilimsikitisha sana mama watoto hawa.
6. Chumbani watoto kuna takataka kila aina.
7. Meli Waingereza ilitia nanga katika bahari Hindi.
8. Uhuru..... watumwa haukupatikana mpaka Waingereza walipofika.
9. Afya watoto hawa si nzuri kutosha.
10. Kusoma watoto hawa hakuridhishi.

B. Yapange maneno haya katika mafungu yanayopatana.

Kwa mfano: *mtoto, mwalimu, mgeni*. ni fungu moja kwa sababu ni majina katika darasa la m-wa (1/2) la nomino za Kiswahili (*tazama habari za sarufi kwanza*).

mtoro	vitanda	pahali	goma
mahali	sanduku	mabuzi	
chakula	mifuko	ufa	rafiki
mkurugenzi	mbuzi	kondoo	madege
kiwanda	chura	kijito	vitoto
ukuta	dirisha	matunda	majitu
ndizi	milima	wazee	buzi
wasemaji	babu	simba	marafiki
mtalii	darasa	somo	mababu
embe	mzizi	majia	vijembe

C. Jaza nafasi hizi kwa kutumia umbo sahihi la neno lililo katika alama za ()

1. Waimbaji waliimba(-zuri) lakini walicheza —(baya).
2. Ni(-gumu) kupata kazi siku hizi hata kama una digrii.
3. Mbwa alibweka(-kali) aliposikia keelele nje ya mlango.
4. Alitembea(polepole) kwa sababu yeye ni kilema.

5. “Kimbia(upesini)”, mwalimu alisema.
6. Kama hutakula(taratibu) chakula chako hakitakufaa.
7. Kutembea(haraka) kunasaidia damu kusafiri katika sehemu za mwili.



MAISHA YA NYUMBANI

Zuhura alianza kuwasimulia wenzake habari za nyumbani, akawaambia, "Mimi naitwa Zuhura. Baba yangu ni Juma, na mama yangu ni Fatuma. Ninaye dada mmoja, kwa jina Habiba na kaka ni Hasani. Sote tunakaa katika kijiji cha Lukuledi katika wilaya ya Masasi. Katika kijiji chetu, watu wote, hufanya kazi pamoja. Lakini, karibu na nyumba yetu pana bustani yenye mipapai, michungwa na maua mazuri.

Kila siku baba pamoja na wenzake huenda shambani kulima na kupalilia. Mimi na dada yangu huenda shuleni. Hasani hajaanza shule, yeye ni mtoto bado. Labda ataanza mwakani.

Asubuhi tunapoamka, mama hufagia nyumba na jiko. Sisi hufagia kiwanja. Halafu mama hupika uji. Baada ya kula chamshakinywa, sisi husafisha vyombo vya chakula. Tunawaaga baba na mama kabla ya kuondoka kwenda shule. Sisi hatuendi shuleni kwa motokaa. Tunatembea kwenda shuleni. Siku nyingine tunakimbia wakati wa kwenda shuleni kwa sababu tunataka kuwahi. Si vizuri kuchelewa shule.

Jioni tunaporudi kutoka shuleni, huwaamkia baba na mama. Mama hutia maji katika beseni kubwa na kuyaweka uani. Humpa baba taulo aji-futie mwili baada ya kuoga. Baba anapomaliza kuoga, mama humwogesha mdogo wetu, Hasani. Sisi huoga wenyewe mtoni.

Baadaye, jua linapokuchwa, mama hupika ugali. Sote hula pamoja. Kama wageni wanafika hukaribishwa. Mbwa wetu Susu naye hula katika bakuli lake. Susu ni mbwa mzuri sana, hulinda nyumba yetu. Kama kuna mgeni hubweka kwa sauti kubwa.

Baada ya chakula, baba huenda kuzungumza na wenzake. Mama hukaa nasi na hutusimulia hadithi. Pia anapenda sana kusuka mikeka ya ukindu. Mimi na Habiba tumeanza kujifunza kusuka kili. Twatumia mikeka hiyo kwa kulalia nyumbani. Mengine mama huiyuza na akipata fedha hununulia vitu vingine. Mwezi jana mama alinunua kuku wa kufuga. Sasa kuku ameanza kutaga na baada ya muda mfupi tutakuwa na vifaranga. Mwishowe tutakuwa na kuku wengi wa kututagia mayai.

Siku za Jumapili sisi tunafanya kazi pia. Humsaidia mama, kuchota maji, kupika mikate na kutayarisha mavazi yetu ya shule. Tunazifua nguo

zetu, tunazipiga pasi na kama zimepasuka mama huzishona. Mama hana cherehani. Kwa hivyo, yeye hushona kwa mkono akitumia sindano maalum.

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu maswali haya

1. Kuna watoto wangapi katika familia ya Zuhura? Taja majina yao.
2. Baba na mama wanafanya kazi zinazofanana?
3. Zitaje kazi wanazofanya baba na mama.
4. Mbwa ana kazi gani katika nyumba?
5. Mama Zuhura anafanya shughuli gani zinazompatia fedha?
6. Unafikiri watoto wanajifunza mengi kutoka kwa nani katika familia?
7. Toa sababu ya jibu lako la (6) hapo juu.

Tumia maneno yafuatayo katika sentensi nzuri

palilia	wahi	beseni
uani	kuchwa	bweka
suka	ukindu	kili

Kazi Maalum

Wanafunzi wasimulie jinsi watu wanavyoishi katika sehemu wanazotoka.

HABARI ZA SARUFI

A. Irregularity in noun classes

Consider the following nouns which designate living things.

afisa	maafisa (5/6)
kipofu	vipofu (7/8)
jemadari	majemadari (5/6)
rafiki	marafiki (5/6)
chura	vyura (7/8).

With the exception of **rafiki**, these nouns follow the agreement rules of nouns in the **m/wa** class. **Rafiki** behaves like the human nouns in class 9/10. Some speakers use this observation as a basis for not using **ma** to indicate the plural form of **rafiki**. This minimizes the problems of shifting from class 6 to class 10 to class 2.

For example:

singular: **rafiki wa/ya Juma.**

plural: **rafiki/marafiki wa** (cl. 2)/**za** (cl. 10) **Juma** (but not **marafiki ya** (cl.6) **Juma**)
 singular **rafiki mzuri** (cl. 1) (and not **rafiki zuri** (cl. 5) or **nzuri** (cl. 9))
 plural **rafiki/marafiki wazuri** (cl. 2) (and not **marafiki mazuri** cl. 6))

B. Diminutives

These are formed with the help of the **ki/vi** prefixes and express the concept of 'small', 'tiny'. Depending on the context, it may be interpreted pleasantly or derogatorily. There are rules for the formation of diminutives.

1. With noun roots of more than one syllable take **ki/vi**
 For example:
m - toto → kitoto/vitoto
2. If the noun root is monosyllabic or begins with a vowel, it will take **j/ji** as well as the diminutive prefix.
 For example:
m - tu → kijitu/vijitu
ua → kijiua/vijiua
j - embe → kijembe/vijembe
3. Nouns of the **ki/vi** class form the diminutive by adding **ji**
 For example:
ki - tabu → kijitabu/vijitabu
4. A derogatory meaning may result from a diminutive noun if **ji** is added.
 For example:
kitoto → kijitoto "a bad, unpleasant kid."
kijitu is considered pragmatically derogatory because **mtu** is a higher form of being and is therefore a respectful form. The diminutive form is, therefore, considered disrespectful.

In general, nouns in the diminutive form follow the agreement rules of **ki/vi** even the nouns designating a person or a living being.

For example:

(a) **Kijitu hiki kina matata sana.**

"This thing (usually a person) is full of mischief."

(b) **Kiua kile kina harufu nzuri.**

"This flower (very tiny one) has a good scent."

Sometimes **ka** is used as a diminutive form instead of **ki**. Thus, **katoto kazuri**.

Kajitu haka kana matata sana.

"This thing (usually a person) is full of mischief."

C. Augmentatives

Augmentatives are formed with **ji /ma** prefixes to give the noun an augmentative meaning with respect to size, number, and character. The formation rules follow those of nouns in the **ji /ma** class (cl. 5/6). However,

1. where the root is monosyllabic or begins with a vowel, the prefix is **j/ji** for the singular and this prefix is retained in the plural.

For example:

m - tu → jitu → majitu

ch - ungu → jungu → majungu

2. noun roots of more than one syllable do not take the **ji** prefix in the singular. However, the plural is formed by the **ma** prefix.

For example:

m - toto → toto → matoto

paka → paka → mapaka

There are a few exceptions and these have to be treated as idiosyncracies in the language.

For example:

nguzo → jiguzo → majiguzo.

The following exemplify the N/N class in which the nasal is assimilated to the following consonant.

For example:

N - buzi → mbuzi

N - dege → ndege

N - jia → njia

N - goma → ngoma

Thus, the augmentative form is formed by rule 2 above.

mbuzi → buzi → mabuzi

ndege → dege → madege

njia → jia → majia

ngoma → goma → magoma

(cf. **goma/magoma** 'bark of a tree' This is a regular form.)

Other rules of agreement follow those of the *ji/ma* class.

For example:

Jitu hili linanisumbua kila siku.

Majitu haya yananisumbua kila siku.

Toto hili halina adabu hata kidogo.

Matoto haya hayana adabu hata kidogo.

The meaning of both the singular and plural forms is often derogatory.

D. Collectives

Some nouns which appear in the *u* (cl. 11) and *n* (cl. 9) class have two plural forms.

For example:

unyoya → **nyoya/manyoya** (11-10/6)

rafiki → **rafiki/marafiki** (9-10/6)

samaki → **samaki/masaki** (9-10/6)

babu → **babu/mababu** (9-10/6)

mama → **mama/wamama** (9-10/2)

The plural form in *ø/n* express a general plural, while the plural form in *ma* or *wa* express collectiveness. The *ma* of augmentative and the *ma* of collectiveness do not correspond. Context can be used to disambiguate them. That is, if the general interpretation of the statement implies derogatory, then *ma* would imply augmentative. Otherwise it would imply collective. Thus the *ma* prefix of **majitu** and **matoto** which is a marker of augmentation also implies a derogatory meaning.

MSAMIATI

beseni	basin.
-bweka	make noise similar to that made by a dog.
cherehani	sewing machine.
fagia	sweep.
-fua	wash clothes with water and soap, also forge metal.
-futa	wipe.
-hukumiwa	be convicted.
(ki)wanja	field, piece of unused land.
kuchwa	past sun set, dusk (cf. <i>kucha</i> to dawn).
maendeleo	progress, development, advancement.
matata	chaos, mess, perplexity.

msamiati unaendelea

(ma)vazi	dress, garment.
(m)keka	mat.
mkurugenzi	director.
(m)tekeleza,ji	a person who implements, one who carries out duties.
mtoro	escapee.
mwakani	in the following year.
nanga	anchor.
nguzo	pilar, post.
-oga	take a shower/bath.
-palilia	weed, cleaning ground under cultivation.
pasi	iron (piga pasi = iron clothes)
-shona	sew.
sindano	needle.
-suka	weave, plait.
-sumbua	disturb, trouble.
-taga	act of laying eggs.
takataka	trash, rubbish.
taulo	towel.
-tunukiwa	be awarded, be endowed.
uani	enclosure, or backyard attached to the house.
ufa	crack on a wall or surface.
ugali	stiff porridge made from maize meal.
uji	porridge.
ujuzi	experience, technique, expertise, knowhow.
(u)kili	a narrow length of plaited leaf-strip of palm, when put together form the mats called mkeka.
(u)kindu	dry palm leaves used for plaiting mats.
(vi)jakazi	female slave.
(vi)faranga	chicks.
wasemaji	speakers.
-wiana	resemble, be of equal status, balance.

SOMO LA NNE

MAZOEZI MAALUM

A. Kamilisha sentensi hizi kwa kutumia 'o' ya uhusiano (relative pronoun)

1. Vyombo ali.....nunua havifai kutumiwa katika nchi za joto.
2. Uhuru ana.....zungumzia ni uhuru wa bendera.
3. Mahali tuta.....fanyia sherehe ni hapa.
4. Mila na desturi mli.....taja ni za nchi gani?
5. Panya wana.....wasumbua wakulima huanza kutokea baada ya masika.
6. Aliwaleta wageni wali.....fika jana.
7. Tuletee motokaa zita.....weza kupanda milima hii bila matatizo.
8. Wanakunywa maziwa yali.....oza.
9. Milima hii ni ile tuli.....sikia kwamba ina madini za kila aina.
10. Walitumia wanyama wali.....letwa kutoka bara kwa shughuli za utafiti katika maabara yao.

B. Badilisha sentensi 1-10 hapo juu kwa kutumia 'amba-'

C. Ziandike sentensi 1-10 kutoka fungu A kwa kukanusha (tazama habari za sarufi kwanza)

Ufahamu

MALEZI YA WATOTO

Neno la kwanza analotamka mtoto ni "mama". Mtoto huongozwa na mama yake. Nyumbani, mama huwa kama mvuto wa smaku katika nyoyo za watoto wake. Mama ni mfano wa nyota ya uongozi katika maisha ya wanadamu wote. Ukubwa wa kazi anayoifanya mama mmoja ni sawa sawa na kazi ya waalimu wote watakaoya jenga maisha ya mtoto baadaye.

Uongozi wa mtoto huanza siku anayozaliwa mtoto. Maumbile ya mtoto hujengwa na yale anayoyaona kila siku. Hutumia anayoyasikia, na anayoyaona kama ni mfano wake wa kuiga. Kutokana na mifano hiyo, huji-funza tabia, desturi, mila na utamaduni wa namna ya kusema na kuwasil-

iana na wanadamu wengine. Kwa hivyo, mama ni mwalimu wa kwanza na ndiye mwenye jukumu kubwa kwa maisha ya mwanaye. Nyumba ya mama ni shule ya kwanza ya mwanaye. Katika nyumba hiyo, mtoto anajifunza subira, ustahimilivu, nidhamu, umuhimu wa kazi, na utiifu. Kwa hivyo, ni kweli kusema kwamba mtoto kabla ya kwenda shuleni huwa ameshajifunza mambo mengi ya maisha yake. Hata baada ya kwenda shule, msaada wa mama bado unahitajika. Mama ndiye anayemfundisha mwanaye uangalifu katika masomo yake na kazi mbalimbali. Humwonya juu ya marafiki wabaya na kumshauri juu ya marafiki wema.

Mwalimu humfundisha mtoto masomo ya vitabuni na humsaidia mtoto kuyaoanisha na yale ambayo alifundishwa na mamaye. Kwa hivyo, kama mtoto hana malezi bora, hawezi kufanikiwa katika mambo mengine. Kuna methali isemayo, "Mtoto unavyomlea, ndivyo anavyokua." Hii ni kweli, kwa sababu ubovu wa tabia ya mtoto huanza nyumbani na sio shuleni. Kama mtoto anafuata njia za marafiki wabaya, ni budi mama kumkanya mapema kabla hajazoea tabia hizo mbaya. Kuna methali nyingine isemayo, "Udongo upatize ungali maji". au, "Fimbo ikunje ingali mbichi."

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu maswali yafuatayo

1. Mtoto huyapata wapi mafunzo yake ya kwanza?
2. Kuna tofauti gani baina ya mafunzo ya nyumbani na yale ya shuleni?
3. Kama mtoto ana tabia mbaya, nani alaumiwe?
4. Taja methali ambazo hutumiwa kuonyesha malezi bora ya watoto.
5. Chagua methali moja, na andika hadithi fupi kuifafanua methali hiyo.

Tumia maneno haya katika sentensi kuonyesha maana yake kamili

tamka	nyoyo	nidhamu
maumbile	iga	utiifu

Kazi Maalum

Wanafunzi wazungumze juu ya tofauti zilizopo baina ya wajibu wa baba na mama katika familia zao.

HABARI ZA SARUFI

The Relative form

Relativization in Swahili takes two forms. Either by attaching the relative pronoun on **amba-** or by inserting the relative pronoun between the tense and the verb root. In cases where the object marker is also present, the object marker follows the relative pronoun.

For example:

aliyepiga.

aliyempiga.

The relative pronouns are similar to the demonstrative form **o** used as a deictic. For living beings, the singular form is **ye**.

There are tense/aspect restrictions when the relative pronouns are used. The relative pronoun may be inserted in the verb form only if the verb has the **na**, **li**, and **ta** tense markers. With **me** tense, and the conditional tenses (cf. Lesson 11) the relative form may be used by attaching it to **amba-**. The relative form cannot be used when the verb has the aspect marker **-ka-** which is used in narratives to indicate subsequent actions (cf. Lesson 9). Notice that the future relative tense is **-taka-**. This is generally the full form for the future tense. The short form **-ta-** is reserved for the simple future while the full form is commonly used with the future relative tense and implies "to be on the point of".

Negating the verb of a relative clause.

There are two ways a verb of a relative clause can be negated:

1. Where the relative pronoun is attached to **amba-**, negation follows the regular negative formation rules.

For example:

a. **Mtu ambaye alifika.**

b. **Mtu ambaye hakufika.**

c. **Mtu ambaye anafika.**

c. **Mtu ambaye hafiki.**

2. Where the relative pronoun is an integral part of the verb morphology, **-si-** is introduced to the verb form, and follows the subject marker. The structure will also lack tense marking irrespective of the implied time reference. For example:

a. **Mtu atakayefika.**

- b. Mtu asiyefika.
- c. Mtu anayefika.
- d. Mtu asiyefika.

Notice the ambiguity that may result. The context will disambiguate. Otherwise, to impress on the time, **amba-** is used. The negative **si** can only be used where the time reference is either in the present and expressed by **na** or in the future and expressed by **ta**. With other time references only **amba** may be used.

MSAMIATI

-iga	imitate, copy, mimic, caricature.
jukumu	responsibility.
-kanya	rebuke, forbid.
lea	bring up a child, nurse, rear.
masika	season of heavy rain
(ma)lezi	nurturing, rearing, bringing up.
(ma)umbile	character, personality.
(m)vuto	a pulling force.
nidhamu	behaviour, manners, etiquette.
nyoyo	hearts (pl. of <i>moyo</i>).
-oanisha	marry, cause to be in harmony/in line with.
-ongoza	lead.
onya	make one see his mistakes, warn, admonish, reprove
oza	rot, go bad, putrefy.
smaku	magnet.
subira	patience, endurance.
-tamka	pronounce, speak out, say.
ustahimilivu	endurance, patience.
umuhimu	importance, need for.
utiifu	obedience.

SOMO LA TANO

A. Sahihisha sentenzi hizi

1. Mwanamke alikwenda duka kutununua mahitaji yetu.
2. Hii ni ng'ombe ya nani?
3. Maneno nilikwambia ni ya kweli kabisa.
4. Ng'ombe yetu amepotea.
5. Mimi nilimsema alale vizuri.
6. Vifo imezidi katika mji yetu.
7. Mti huu huwezi kuanguka.
8. Nilikwenda katika Nairobi kwa sababu ya kuwa kumwona wazazi.
9. Wachezaji kwa mpira wa miguu ni hapa.
10. Wavuvi walikuwa pumzika karibu na bahari.

B. Badilisha sentenzi zifuatazo katika kauli ya kutendewa

Kwa mfano:

Mimi ninampenda sana mama yangu.

Mama yangu anapendwa sana na mimi.

1. Watoto watapika chai ya asubuhi.
2. Walimwendea mwalimu wao ofisini kwake.
3. Atasema habari zote.
4. Atakulazimisha kunywa chupa tatu za bia.
5. Watu huzungumza Kiingereza sehemu nyingi duniani.
6. Atachukua pesa zote atakapofika.
7. Atamfunga kamba miguuni.
8. Mama alizaa mtoto mzuri hospitalini.
9. Jaji aliamua kesi bila shida.
10. Walitengeneza motokaa yake lakini bado ni mbovu.

Ufahamu

USAFIRI UNGUJA

Mara nyingi babu zetu hutushangaza kwa hadithi za kale. Baadhi ya wakati huwa ni mtindo wa kutaja mambo ambayo hayapo. Siku moja alizuka na kusema, "Zamani Unguja kulikuwa na magari ya farasi!. Yalikuwapo ya kukokotwa na farasi mmoja mmoja, wawili wawili na hata wanne kwa pamoja.

Sikupenda kumkaidi ingawa mimi katika kufungua macho yangu nimeona magari ya ng'ombe na punda tu.

Siku nyingine akasema, Unguja ilikuwepo reli, ikipakiwa abiria na mizigo. "Hee, hata reli!" nilisema kwa mshangao. Hata babu alishtushwa kwa jinsi nilivyostaaajabu.

"Nadhani unaona hayamkini kwa kisiwa kidogo kama hiki kuwa na usafiri wa namna hiyo. Kwa kweli, reli ilikuwapo na ilidumu kwa kiasi cha miaka ishirini na tano hivi. Ilikuwa ikiondokea hapa Forodhani mjini na kwenda Bububu, ambako ni kilometa kumi na moja kuelekea kaskazini. Ingawa masafa hayo si marefu, na safari ni fupi lakini kulikuwa na vituo vingi vidogo vidogo kati yake ambavyo abiria pamoja na mizigo yao hupanda na kuteremka. Vituo hivyo ni pamoja na Malindi, Gulioni, Saateni, Sharifu Musa, na Kibweni."

"Treni hiyo ilikuwa ikienda na kurudi kutwa mara nne. Katika muda wote huo wa kukaa kwake haikupata kutokewa na hatari ya kugongana wala kupinduka. Sababu ni kuwa haikuwa ikipishana na treni nyinginezo wala haikuwa na mabehewa mengi ila matano tu, ya abiria na mizigo. Kwa jumla safari za reli hii zilikuwa na raha sana kwa abiria. Njia yake ilisadifu kupita karibu na pwani, kwenye upepo maridhawa wenye kuburudisha joto la jua kali."

"Kadhali, rangi ya buluu ya bahari ilivutia na sauti za mawimbi yakisukumwa na upepo wa maleleji ziliwatumbuiza abiria. Kwa upande wa pili, kulikuwa na mandhari nyingine tofauti. Reli hii hii ikipita chini ya vivuli vya miti kama minazi na miembe iliyonawiri na kukoza kwa rangi zake za kijani. Fursa zote hizi zikipatikana bila abiria kupunjana kwani mabehewa yao yalikuwa yakiachwa wazi sana ili mwangaza uenee ndani kwa nafasi."

"Mwisho wa safari zake, treni hii ililala Ngome Kongwe. Humo vile vile, ndimo mlimokuwamo kiwanda chake cha kuchongea vipuri pamoja na kufanya matengenezo mengine."

Hii hadithi ya kuwapo kwa reli Unguja na magari ya farasi inakaribia kuwa ni maelezo ya kuchekesha tu, kwa jinsi hali ya namna ya usafiri ilivyobadilika. Sasa zipo gari za aina kwa aina katika kila barabara.

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu maswali yafuatayo

1. Kwa nini mwandishi wa hadithi hii alishtuka?

2. Reli iliyokuwapo Unguja ilidumu kwa muda gani?
3. Kwa nini palikuwa hapajatokea ajali ya treni kwa muda wote huo?
4. Safari ya treni ilipitia vituo gani?
5. Taja umuhimu wa kituo cha Ngome Kongwe.
6. Kwa nini mwandishi anasema kwamba safari ilikuwa ya raha sana?

Tafuta maana ya maneno yafuatayo kulingana na yalivyotumiwa katika hadithi.

abiria	maridhawa	behewa
kiwanda	maleleji	vipuri
mandhari	fursa	kudumu
kushtuka	kustaajabu	masafa
kusadifu	kutumbuiza	kunawiri

Kazi Maalum

Wanafunzi wazungumze juu ya safari waliyofanya na ambayo iliwapendeza

HABARI ZA SARUFI

The Passive form

The passive is indicated by inserting **w** before the final vowel **a**. The subject of the active verb is replaced by the object which changes its grammatical role to the subject of the passive verb. The old subject becomes redundant, but may optionally appear at the end of the construction with the **na** of association. The two will form a prepositional phrase equivalent to the English "by" phrase. In the case of an instrument, the prepositional phrase will have **kwa** instead of the **na**.

For example:

Alipigwa na mama.

Alipigwa kwa fimbo.

Depending on the meaning of the verb root and common usage, most Swahili verbs can take the passive form.

1. Verbs which form the passive by inserting the **w** before the final vowel include:
 - (a) verbs with **-a** as the final vowel in the finite form. This includes most of the verbs of Bantu origin.

- (b) verbs in which the final vowel is preceded by a consonant or a vowel **e** or **i**.

For example:

pika → pikwa

pokea → pokewa

tia → tiwa

2. Other verbs of Bantu or Arabic origin take the passive form of the “applied” (also called “prepositional”, “directive”, “-i- extension”) form of the verb. This includes also the verbs that are already extended by the applied forms: **-ea, -ia, -lia, -lea**.

For example:

Bantu:

chukua → chukuliwa

ondoa → ondolewa

la → liwa

pa → pewa

Arabic

badili → badiliwa

samehe → samehewa

verbs with applied forms:

pikia → pikiwa

zalia → zaliwa

somea → somewa

ondolea → ondolewa

MSAMIATI

abiria	passenger(s).
-burudika	be refreshed, comforted, be cooled.
-chonga	carve, make from wood or metal by carving or forging.
-dhani	think, suspect, guess.
-dumu	last, survive hard conditions.
-gongana	collide, bang on each other, hit on each other.
farasi	horse.
hayamkini	impossible (yamkini = possible).
jaji	a judge.
-kaidi	contradict, be obstinate, be head-strong.
kesi	lawsuit, case (criminal or civil).
-kokota	drag, pull along, haul, draw (a cart).
-koza	be well seasoned, have the right amount of color/seasonings.
kutenda	to do, (in grammatical terms "active").
kutendewa	to be done to (in grammatical terms "passive").
maleleji	season of uncertain and changing winds.
(ma)behewa	between the monsoon and during the rains.
mandhari	compartment or carriage of a train.
maridhawa	environment, landscape, physical features of the land.
(ma)wimbi	in abundance, plenty, sufficient.
(m)shangao	wave, tide.
(m)tindo	amazement, bewilderment (cf. -shangaa)
(m)zigo	style, mannerism, way of doing something.
-nawiri	load, luggage.
-pakia	look healthy, nourished, attractive.
-pinduka	load onto (cf. <i>pakua</i> - unload).
-punja	turn over, overturn.
-sadifu	give short measure, give less than is due, cheat, swindle.
-staajabu	turn out to be good/well/proper/right/exact.
-teremka	wonder, be astonished, feel surprise.
-tumbuiza	descend, climb/slide downwards.
(vi)puri	entertain with music.
-vutia	spare parts.
-zuka	attract, interest.
	appear suddenly, emerge, pop up, invent for.

SOMO LA SITA

MAZOEZI MAALUM

A. Jaza nafasi hizi kwa kutumia neno -faa


Kwa mfano: *kiti: kiti kifaacho.*

1. Yeye ni mwalimu
2. Alimpa pesa matumizi ya mwezi mzima.
3. Sentenzi hizi, si kuonyesha maana kamili ya maneno haya.
4. Walichagua nchikupewa msaada wa kimataifa.
5. Hayo ni maazimio kwa maendeleo ya nchi.
6. Je, walizileta meza?.
7. Hawakuweza kupata msaada
8. Mnaweza kuleta kitu chochote kwa sherehe.
9. Walipanda miti kwa utoaji wa mbao za ujenzi.
10. Mbuzi huyu, ndiye kuchinjwa.


B. Yafuatayo ni majina ya sehemu za mwili. Vionyeshe viungo hivi katika picha. Halafu, yapange majina haya katika mafungu kulingana na madarasa ya nomino za Kiswahili

sikio	nywele	pafu	kisogo
kivi	jicho	kitovu	paja
pua	kwapa	kidevu	mdomo
utosi	taya	kifundo	goti
uwayo	shingo	kiuno	mgongo
moyo	utumbo	figo	koo
tako	bega	kifua	mbavu
kidole cha pete	kidole gumba	kisigino	
vidole vya mguu	vidole vya mkono	panda.	

Sehemu za mwili wa binadamu



Sehemu za mwili wa binadamu



Ufahamu

MATUMIZI YA LUGHA

Watu wengi huko Afrika wana bahati ya kuzungumza lugha mbili au tatu. Katika sehemu moja iitwayo Usangi huko Tanzania, wenyeji wanasema lugha tatu maalum ambazo ni Chasu, Kiswahili, na Kiingereza. Kati ya lugha hizi tatu, ipendelewayo zaidi ni Chasu, ambayo ni lugha mama ya wenyeji wa Usangi. Inaonekana ni lugha ya kwanza kwa watu wa Usangi kwa sababu watu wa Usangi ambao hawajaenda shule, kama vile wazee, na watoto wadogo, hawafahamu lugha nyingine isipokuwa Chasu.

Kiswahili ni lugha ya kufundishia. Huko Usangi, zamani watu walijua Chasu tu kwa sababu palikuwa hakuna mtu ye yote ambaye alikuwa anawafundisha Kiswahili.

Lugha ya Chasu hasa, hutumika nyumbani, njiani hata madukani. Kiswahili kinatumika katika miji mingine mingi ambayo ina Waswahili au watu wajua Kiswahili. Kiswahili kinatumika sana Tanzania kwa sababu ni lugha ya Taifa, ambayo inatumika katika shule, shughuli za biashara, shughuli za dini, shughuli za serikali na mahali pengine pengi.

Kiingereza ni kigumu sana, kwa watu wa Chasu na Tanzania nzima. Lugha hii hufundishwa shuleni. Kwa kawaida hupewa vipindi vitatu au vinne kwa juma. Lakini, wanafunzi hawapati nafasi ya kuitumia lugha hii kikamilifu mpaka wamalize masomo ya shule za msingi na kuingia sekondari. Katika shule za sekondari, wanafunzi hufundishwa baadhi ya masomo yao kwa Kiingereza. Hufundishwa somo la Kiingereza pia. Hata hivyo matumizi yake ni kidogo sana ukilinganisha na Kiswahili. Wanafunzi hutumia Kiswahili kwa mazungumzo yao ya kila siku na Kiingereza darasani iwapo mwalimu wao anatumia Kiingereza.

Ikiwa mtu atasafiri nje ya Tanzania, anaweza kujifunza Kiingereza zaidi kwa sababu njia kuu ya mawasiliano ni Kiingereza. Hata hivyo, nafikiri watu wawezao kusema lugha mbili au tatu wana bahati sana. Kujifunza lugha ambayo ni tofauti sana na lugha mama si jambo rahisi. Inahitaji kazi na bidii nyingi. Njia mojawapo ya kuimarisha ujuzi huo ni kusoma vitabu vilivyoandikwa kwa lugha hiyo na kujaribu kuizungumza kila ipatikanapo fursa ya kufanya hivyo.

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu Maswali yafuatayo

1. Kwa kawaida watu wa Afrika wanaweza kusema lugha ngapi?
2. Taja lugha mbili za Kiafrika ambazo unazijua.
3. Wenyeji wa Chasu wanaweza kuzungumza lugha ngapi?
4. Wenyeji wa Chasu wanatumia lugha zote tatu sawa sawa?
5. Mwandishi anasema nini juu ya Kiingereza?
6. Ili kuimarisha lugha, mwanafunzi hana budi kufanya nini?

Kazi Maalum

Wanafunzi watoe mawazo yao juu ya matumizi ya lugha katika sehemu wanazoishi.

HABARI ZA SARUFI

More on Relativization

In Lesson 6, we discussed the two ways a relative pronoun can be used. These are, by attaching it to **amba** or by inserting it into the verb. In this Lesson, we saw cases in which the relative pronoun appears as a suffix on the verb. In such cases, the verb does not have a tense prefix. Thus, the construction carries no time implication. Depending on the context, the interpretation may have a present, future, habitual, or past time reference.

Recall the proverb in Lesson 6:

Mtoto unavyomlea ndivyo anavyokua

Ordinarily this proverb is cited as: (it was changed to suit our purposes in Lesson 6)

Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.

As such it does not have a specified time reference. Suffixing the relative pronoun on the verb is also considered a preferred way to relativize on a verb which has a stative interpretation (cf. Statives in the grammar section of Lesson 13.)

MSAMIATI

baadhi	some, an assortment.
fursa	chance, opportunity.
goti	knee.
gumba	big toe/finger.
-imarisha	strengthen.
kidevu	chin.
kifo	death(cf. kufa).
kifundo	knot, ankle.
kikamilifu	in fullness, completely.
kisigino	heel.
kitovu	navel.
kiuno	waist.
kivi	elbow.
-linganisha	compare.
mawasiliano	communication.
mgongo	back, backbone.
paja	thigh.
panda	forehead.
-ridhisha	satisfy.
taya	jaw, jaw-bone.
utosi	crown of head.
uwayo	palm of foot.

SOMO LA SABA

MAZOEZI MAALUM

A. Jaza nafasi zilizoachwa

1. Ninafurahi —(sikia) kwamba unasoma Stanford.
2. Nani anaweza —(buni) mwalimu anatoka wapi.
3. Aisha alitaka — (eleza) matatizo yake ya nyumbani.
4. Asante kwa mazungumzo, ni lazima — (ondoka) sasa.
5. Nimefurahi —(kutana) nawe, kwa heri ya —(onana).
6. Nilikwenda mjini — (tazama) sinema.
7. Hii ni mara yako ya kwanza —(tembelea) Uingereza?
8. —(cheza) anataka lakini si katika timu hii.
9. Kwa nini —(uliza) maswali kama haya?.
10. Alifika halafu akachukua bunduki yake na —(anza) —(piga) risasi ovyo.

B. Andika miaka hii kwa maneno

1. 1732	6. 586
2. 1485	7. 1870
3. 1653	8. 1215
4. 1923	9. 2049
5. 1097	10. 1968

Ufahamu

UHURU NI NINI?²

Watu wengi wanafikiri kwamba uhuru maana yake ni uhuru kutoka katika utawala wa wakoloni. Lakini kama nchi ni maskini na wananchi wake hawana elimu ya kutosha, ni wajinga na wanyonge, basi nchi hiyo si huru hata kama si koloni la nchi nyingine. Tunasema nchi hiyo ina uhuru wa bendera tu na haina uhuru kamili. Kama nchi haina uhuru kamili, taifa lo lote la kigeni lenye maendeleo na nguvu zaidi linaweza kuhatarisha uhuru wa nchi na wananchi wake. Je wananchi wanaweza kuulinda uhuru wao kwa njia gani? Kwa kujitegemea.

Ni dhahiri kwamba uhuru maana yake ni kutosumbuliwa na njaa, maradhi, na umaskini. Haya yanategemea maongezeko ya mali na elimu nchini;

maana watu wanaweza tu kutumia mali waliyoichuma. Na hata uhuru wa mtu binafsi utakuwa na maana kama shabaha yake ni maendeleo. Mtu anaweza kutetea haki zake bara-bara kama haki hizo anazijua, na anazijua sheria zinazomlinda kitaifa na kimataifa. Nchi, ambayo watu wake wanaelewa mambo haya, ni huru na tunaweza pia kusema kwamba nchi hiyo ina maendeleo. Lakini maendeleo ni nini?

Maendeleo si mabarabara, majumba, kuongezeka kwa mazao, na vitu vingine vya aina hii. Hivi ni vyombo vya maendeleo. Kazi ya barabara ni kumwezesha mtu kusafiri au kusafirisha mazao yake. Kwa hivyo, faida ya barabara mpya ni kumpa mtu uhuru wake wa kusafiri na kusafirisha mazao yake. Kama serikali inaamua kuongeza idadi ya majengo ya shule, itakuwa vizuri kama majengo hayo yanaweza kutumiwa kuongeza ujuzi wa elimu ya watu. Kama wananchi wataongeza mazao kama vile mazaø ya ngano, mahindi na maharagwe ni kwa lengo la kujipatia chakula bora zaidi. Mazao ya biashara yana lengo la kuwapatia wananchi fedha za kununulia vitu vingine vya maendeleo. Kama wananchi wanajitegemea, uchumi wa nchi hiyo utakuwa mzuri pia. Uchumi mzuri utawafanya wananchi kuwa na afya bora zaidi, starehe zaidi, na elimu zaidi. Huu ndio uhuru wa kweli. Maendeleo yasiyokuwa maendeleo ya watu hayana maana kwa Waafrika. Mpiramidi ya misri, na mabarabara ya Warumi yaliyoko Ulaya yalikuwa maendeleo ya vitu ambavyo mpaka leo yanatushangaza. Lakini hayakuwa maendeleo ya watu na sehemu kubwa ya maendeleo na utamaduni wa nchi hizi, imeteketea zamani sana.

Kwa hivyo uhuru ni kujitawala, kujitegemea na kufanya yale ambayo yanawaletea wananchi wengi maendeleo. Mipango ya maendeleo ya nchi lazima iwe na lengo la kuwafaidia watu wengi na kumaliza shida zao. Kila mpango uamuliwe kwa kupima kama unatimiza shabaha ya maendeleo, na shabaha ya maendeleo ni watu.

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu maswali yafuatayo

1. Mwandishi anatuambia uhuru maana yake ni nini?
2. Kama wananchi hawana uhuru wa kweli wanaweza kuwa na maendeleo? Toa maelezo kwa jibu lako.
3. Mwandishi anasema kwamba majengo na mabarabara si maendeleo. Je unakubaliana naye?
4. Mwandishi anasema utajua kama nchi fulani imeendelea?
5. Mazao ya chakula na biashara yanawasaidia je wananchi kupata maendeleo?

6. Kwa kutumia Kiswahili tu, andika maana ya maneno yafuatayo. Unaweza kutumia kamusi lakini zingatia matumizi katika kifungu ulichosoma.

dhahiri	tegemea	lengo
wajinga	wanyonge	silaha
gharama	njaa	maradhi
ongeza	teketea	teseka
shangaza	faidia	amua

7. Chagua maneno matano kutoka (6) uyatungie sentensi.

Kazi Maalum

Wanafunzi watoe mawazo yao kuhusu mada ya "Uhuru"

HABARI ZA SARUFI

The Infinitive Form

There are two basic functions for the infinitive form of the verb in Swahili which have to be distinguished from each other.

- (a) The verbal infinitive as in

Ninapenda kula mihogo. "I like to eat cassava.

This usage is similar to the infinitives in English.

- (b) The verbal noun. This may be considered equivalent to the English gerund form or the infinitive form.

For example:

Kuimba ni kazi ya watoto.

"Singing is children's work."

or

"To sing is children's work."

This usage should be straight forward at this stage of the student's knowledge of the language. We want to concentrate on the usage as exemplified in the exercises at the beginning of this Lesson. The examples show two actions one of which is expressed by the infinitive.

1. A statement introduced by the following adverbial phrases is expressed by the infinitive form of the verb. **baada ya**, **kabla ya**. The following examples are helpful.

Baada ya kusoma, alienda kulala.

“After reading, he went to sleep.”

Kabla ya kusafiri, aliwaambia watoto wake watunze mali yake vizuri.

“Before he travelled, he told his children to take care of his wealth.”

Sometimes **lazima** and **afadhali** are followed by the infinitive form of the verb although the subjunctive form is more regularly used. When the infinitive form is used, the statement receives a general (rather than a specific) interpretation.

Ni lazima kusoma kila siku.

“It is a must to read everyday.”

Ni afadhali kuacha motokaa nyumbani na kutembea.

“It is better to leave the car at home and walk.”

2. When two actions are closely related but the second is not a resultant or subsequent in time to the first, the second action is generally expressed using the infinitive form.

For example:

Walikuja mara moja na kuondoka.

“They came briefly and left.”

3. If an infinitive verb precedes a finite verb form in a construction, the idea in the infinitive verb is given prominence.

For example:

Kulala apenda sana, ni kufanya kazi hapendi.

“To sleep, he likes very much, it is to work that he does not like.”

or

“As for sleeping, he likes very much, it is working that he does not like.”

4. When the infinitive follows the verb of the finite form it emphasizes the main idea in the verb of the finite form.

For example:

Wanaweza kutetea haki zao barabara.

“They can defend their rights effectively.”

5. The infinitive form can be used in a situation where tact is required. As such it is used in an impersonal sense.

For example:

Ninafikiri ni afadhali kuondoka sasa.

instead of

Ninafikiri ni afadhali uondoke sasa.

“I think it is better (for you) to go now.”

It is most helpful in questions that can be interpreted as patronizing.
For example:

Kwa nini kufanya hivyo?

“Why do that?”

instead of

Kwa nini unafanya hivyo?

“Why are you doing that.”

Negative of ku-

The negative of ku- is kuto-. For example in the reading lesson we have:

...uhuru wa kutosumbuliwa na njaa, maradhi, na umaskini.

“The freedom not be troubled by hunger, sickness and poverty.”



MSAMIATI

barabara	broad road, highway
bàrà-bàrà	exactly, quite right, just as it should be, agreed.
barafu	ice.
bendera	flag.
binafsi	self, (<i>mtu binafsi</i> an individual)
bora	good, appropriate, fine, valuable, excellent, high
bunduki	gun.
-chechemea	limp.
-chuma	pick, pluck, reap, harvest, acquire wealth, reap.
dirisha	window.
dola	reign, empire, kingdom, royal government
dhahiri	clear, exact, undoubtedly.
-faidia	profit (cf. <i>faida</i>).
fani	worthy, fitting, prosperous.
haja	need, necessity.
haki	right(s)
hiari	free will.
-husiana	be acquainted, relate.
idadi	amount, measure of countable items.
ijapo	even if, supposing that, although.
kahawa	coffee.
kelele	loud noise.
kifani	unique, equalled, similar to.
kimataifa	internationally
kitaifa	nationally.
lengo	target, intended outcome, aim.
licha	not only....but..
linda	protect, guard.
mada	topic of discussion
madhali	while, since, when, if, seeing that, because.
(ma)haragwe	kind of bean.
mali	wealth, possessions.
(ma)piramidi	pyramid.
maradhi	desease, illnesses, sickness.

msamiati unaendelea

maskini	poor
matata	troubles, confusions, problems.
(m)kongwe	sisal.
(m)kongwe	very old (of a person).
(m)korofi	evil minded, tyrannical, destructive, malignant, brutal.
(m)nyang'anyi	robber.
(m)pango	plan, arrangement, organization.
(m)pishi	a cook.
(m)seja	bachelor, an unmarried man.
(m)taalamu	expert, educated, scholarly, well-informed.
(m)taratibu	careful, orderly, (also quiet, methodical).
mtungi	an earthen pitcher, water jar made of baked earthenware.
(mw)ema	good, pleasant.
-nawa	wash oneself.
ngano	wheat.
njaa	hunger
-panua	open wide, widen, increase the size.
pamba	cotton.
-pima	take measurement, examine, think.
risasi	bullets.
-shangaza	astound, astonish, amaze, dumbfound.
starehe	relaxation, pleasure, enjoyment.
-teketea	be consumed, be destroyed, be ruined.
-tetea	defend, support.
-tumia	use, exploit.
-timiza	fulfil, complete, perfect, finish.
-timka	trot, run (also be ruffled as of hair or feathers).
uchumi	economy.
utamaduni	culture, a way of life.
(wa)jinga	fool, idiot, unwitty, stupid.
(wa)nyonge	weak persons, (unyonge = weakness)
Warumi	Romans.
wazi	open, openly, clear, clearly, obvious.
-zingatia	take into account, consider, take note, include, remember.
-zirai	faint, lose consciousness.
zoezi	exercise.

SOMO LA NANE

MAZOEZI MAALUM

A. Tumia neno sahihi ili kujaza nafasi hizi

ndipo	wa	ni
ndiye	po	nazo
ambayo	sana	

1. Marikani Kaskazini ni sehemu kubwa yenye dola mbili kubwa,ni Umoja wa Serikali za Marikani (USA) na Kanada.
2. Askaripolisi aliyejeruhiwa ndugu yangu.
3. Mombasa bandari kubwa Afrika ya Mashariki.
4. Mwalimu sayanzi,..... ajuaye habari hizi.
5. Hapa akaa..... Meya wa mji huu.

B. Tumia '-pi' ili kukamilisha sentensi hizi

1. Alitaka kufahamu ni mwanamkealiyefika jana.
2. Wanafunzi hawajui darasa ni lao.
3. Alileta mifuko?
4. Unatafuta viatu?
5. Mwambie ni vijana waliofika jana.
6. Ulizaliwa mwezi?
7. Ni zawadi ulizowapa watoto hawa?
8. Kuna uhuru wa bendera na uhuru kamili. Sasa unapendelea?
9. Watoto hao wanapendelea kucheza?
10. Mahali ambapo alitarajia kukaa baada ya kustahafu.

C. Huitwaje?

1. Mtu ambaye hawezi kusema.
2. Mdudu mdogo wa jamii ya nzige.
3. Mtu anayeza vitu dukani au sokoni.
4. Kitabu watumiacho waislamu wakati wa kusali.
5. Watu wanaoshiriki katika michezo mbalimbali.
6. Kiongozi mkuu wa nchi.
7. Mtu mwenye ujuzi wa kuendesha ndege (eroplani).
8. Mtu mwenye ujuzi wa kuendesha meli.
9. Mtu mwenye ujuzi wa kuendesha motokaa.

10. Kitu kitolewacho bila mpokeaji kukilipia gharama.
11. Wakati wa jua kali.
12. Kipindi cha mvua kubwa.
13. Mtu awapikiaye watu wengine, kama vile katika mahoteli.
14. Mtu afuaye nguo kwa malipo ya fedha.
15. Wadudu waonekanao mahali pachafu.

Kutungua sentenzi

Chagua maneno (5) kati ya hayo uliyovumbua hapo juu na uandike sentenzi moja kwa kila moja.

Ufahamu

MASHAIRI

Mashairi yalianza kutungwa zamani sana. Yalitungwa kwa sababu mbalimbali. Mara nyingi kwa kumsifu mtu, kumdhihaki mtu, kwa sababu ya huzuni au furaha ya jambo fulani, na kadhalika. Mashairi yalitungwa ili kuimbwa, lakini siku hizi si watu wengi waimbao mashairi. Hata hivyo, mashairi huimbwa katika redio au katika sherehe mbalimbali.

Katika kujifunza juu ya mashairi, tunajifunza jinsi ya kupanga mizani, beti, vina, vituo, na utoshelezi.

Sasa tutazame shairi lifuatalo:

MKULIMA

**Mkulima zindukana, na mvuvi kadhalika
Ufugaji ndio sana, inafaa kuchemka
Jambo hili la maana, Arusha lilikotoka
Azimio la Arusha, mkulima lima vema**

**Utie mbolea kwanza, uonyeshe ustadi
Shamba lote kueneza, vipimo vimewekwa yadi
Usichojua uliza, wakuonyeshe weredi
Azimio la Arusha, mkulima lima vema**

**Limeni pamba na mboga, na vyakula kadhalika
Wala usiwe na woga, trekita kuzishika**

Mtifu zote mbuga, utajiri kuushika
Azimio la Arusha, mkulima lima vema

Mvuvi nawe sikiliza, usije kuniuliza
Mwalimu kutueleza, yafaa kutekeleza
Inapasa kuyakuza, mabwawa kuyaongeza
Azimio la Arusha, mkulima lima vema

Tunaweza sasa kuutazama muundo wa shairi hili. Shairi hili lina beti nne. Shairi linaweza kuwa na beti nyingi, kutegemeana na anayotaka ku-sema mwandishi. Ubeti ni jumla ya mistari iliyopo katika sehemu moja ya shairi. Kwa kawaida, ubeti wa shairi una mistari minne kama shairi hili linavyoonyesha, na kila mstari una mizani kumi na sita. Kwa mfano mstari wa kwanza wa ubeti wa kwanza:

M-ku-li-ma zi-ndu-ka-na, na m-vu-vi ka-dha-li-ka.

Vina vya shairi ni silabi ya kati na ya mwisho katika kila mstari wa ubeti. Katika shairi hili, kila ubeti una vina vyake. Kwa mfano, ubeti wa kwanza, vina vya kati ni *na*, na vina vya mwisho ni *ka*.

Mstari wa mwisho wa ubeti huitwa kituo. Kituo kina kazi moja maalumu, kuonyesha mwisho wa ubeti. Kama mstari wa mwisho wa kila ubeti wa shairi zima ni sawa, kituo kinaonyesha kiini cha shairi zima. Kwa mfano, kiini cha shairi hili kinaonyeshwa kwa mstari wa mwisho kurudiwa katika kila ubeti. Mwandishi anawahimiza wakulima walime vema. Kina cha kati cha mstari huu ni *sha*, na kina cha mwisho ni *ma*. Kujitosheleza kwa shairi maana yake ni kila ubeti kuwa na maana yake kamili bila kutegemea ubeti unaotangulia au unaofuata.

Mashairi mengi huandikwa kama shairi la hapo juu.

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu maswali haya

1. Mshairi anaweza kuwa na madhumuni mbalimbali ya shairi analotaka kuandika. Yataje.
2. Zamani mashairi yaliandikwa ili.....
3. Shairi huwa na vipengele vifuatavyo: ubeti; vina; mizani; kituo. Kwa kutumia shairi hili, vifanue vipengele hivi.
4. Vina vya shairi zima ni sawa? Thibitisha jibu lako.

Kazi Maalum

Wanafunzi watafute shairi moja fupi na kulifafanua darasani wakionyesha mwandishi anasema nini katika shairi hilo. Ifuatayo ni orodha ya makala ya ushairi ambayo wanafunzi wanaweza kutumia.

1. Pambo la Lugha : *Shaaban Robert, 1968. Oxford Press, Nairobi.*
2. Sheria za kutunga mashairi : *Abedi K. Amri, 1973. EALB. Kampala.*
3. Mashairi ya Mfungo wa Ramadhani : *Sengo, T. S. Y., 1979. EAP. Arusha.*

MSAMIATI

beti	verse.
-dhihaki	ridicule, mock, deride, make fun of.
-enea	spread, cover a large area.
-fafanua	explain, describe, clarify.
huzuni	sadness.
-jeruhi	injure.
kina	rhyme, final syllable.
kituo	stop, pause, a note of punctuation.
-kuza	make grow, cause to get bigger.
(ma)dhumuni	intention.
mbuga	steppe.
meya	mayor.
mizani	meter.
muundo	structure.
nzige	locust.
sahihi	correct.
sherehe	celebration.
silabi	syllable.
-tekeleza	take action, carry duties through.
-tekeleza wajibu	carry out responsibilities.
-tifua	make dust, cause to rise like dust.
-tunga	compose.
utoshelezi	sufficiency, adequacy, satisfaction.
ustadi	skill, expertise, capability.
weredi	skill, cleverness.
woga	fear, a scare.
-zindua	remove something fixed firmly, set free from a spell. Also used to mean inaugurate.
-zinduka	come out of a spell or trance.

SOMO LA TISA

MAZOEZI MAALUM

A. Kamilisha sentenzi zifuatazo kwa kutumia neno lifaalo kati ya haya yaliyomo katika alama za vifungo ()

1. Ukienda kuoga ni budi nguo zako kwanza (ufue; uvue).
2. Moto hauwaki wala moshi (haufuki; hauvuki).
3. Leo nguo zake rasmi (hakuvaa; hakufaa).
4. Ametajirika kwa mali ya baba yake (kurithi; kuridhi).
5. watu wengi pana kelele nyingi pia (kwenye; penye).
6. nisaidie kwa sababu nina shida kubwa sana (tafadhali; afadhali).
7. Nilimwambia nisemayo (asikie; asikilize).
8. Alikuwa hana aliyemwibia pesa zake ni jirani yake (shaka, - mashaka).
9. Nchi zetu hazikubali kutoa hata moja ya ardhi kwa mabepari (nchi, inchi).
10. Baada ya kupika mama ali..... chakula na kuwapa watoto (pakua; pakia).

B. Malizia sentensi hizi kwa kutumia 'ka'

1. Aliamka, halafu(kula) chamshakinywa.
2. Maharamia walikivamia chombo, kisha(pora) mali yote iliyo-kuwemo.
3. Musa alivuta kiko chake mara mbili, tatu, ndipo(eleza) inspekta wa polisi mambo aliyokuwa ameyaona pangoni.
4. Nenda kwanza(ona) mzee wako akupe maoni yake.
5. Kwanza aliapata shahada ya juu ya uhandisi, halafu(enda) kufanya kazi huko Afrika ya Mashariki.

C. Tafsiri kwa Kiswahili

1. First, the lady was surprised at hearing this, and then began to question the boy.
2. He attended the meeting, and then left for his home town.
3. The dog continued to look for the animal and then suddenly it heard the lion roaring.
4. The parents arrived, then the ceremony began. It went on for a while, and then someone entered from the back door. He announced that the wedding should not take place.

5. Everyone was astonished at this announcement, and they just looked at the man until the bride's father approached him and asked him, "What do you want from my family?" He then answered, "Everyone knows that this is my legal wife."

Ufahamu

ADUI WA WAKULIMA

"Mazao yote yanaliwa"! alisema Matiko. "Nani amekula mtama wetu?" "Nani amekula matango yetu?" "Nani amemaliza mahindi yetu?" Aliuliza Matiko. "Kama ni mtu, lazima anyongwe."

Mnyonyaji hula kitu asichopanda. Mtu anayekula vya wenzake tu bila kufanya kazi ni mnyonyaji. Ni adui yetu. Hatumtaki mnyonyaji katika nchi yetu. Katika nchi inayotaka kuendelea, lazima kila mtu afanye kazi.

Matiko aliporudi nyumbani alionekana mwenye huzuni sana. Baba yake akamwuliza, "Mbona leo una huzuni?" "Una nini" Matiko akajibu, "Wanyonyaji wamefika shambani kwetu. Wamekula mahindi, mtama, na matango yote. Nafikiria njia ya kuwakamata wevi hawa." Baba yake aliposikia hivi alimsifu Matiko. Alijua kwamba mwanae sasa amepata akili ya kujitegemea. "Twende tukawawinde", alisema baba yake Matiko. "Unawafahamu?" aliuliza Matiko. "Ndio, ni ngedere" alisema baba yake. Kisha akaendelea, "Kila mwaka tunapata taabu ya kuamia mashamba yetu. Ngedere ni wanyama wabaya sana. Ni wezi wa mazao yetu, ni adui wa binadamu.

Matiko alifurahi kusikia hayo, akawaambia rafiki zake Dihani, na Mashaka Siku ya Ijumaa, wakaenda porini kuchonga silaha. Matiko alichonga rungu kubwa sana, Dihani akakata gongo la urefu wa meta moja, na Mashaka akachonga upinde na mishale. Kule nyumbani walimwacha baba yake Matiko anasafisha bunduki yake. Mama na dada yake waliwapikia mabumunda ya kula watakapoenda kuwinda. Mabumunda ni mikate ya ndizi na unga.

Jumamosi asubuhi walikunywa uji, na kila mmoja akala bumunda moja. Yaliyobaki waliyafunga vizuri na kuyatia katika mikoba. Baba yake Matiko alitangulia akibeba bunduki yake na mfuko wa risasi. Nyuma yake alikuwa Matiko na rungu lake, na halafu Mashaka na Dihani na silaha zao. Wote walionekana kama askari hodari waendao vitani. Kweli hii ilikuwa vita baina ya ngedere na mwanadamu.

Wakaingia msituni kimya kabisa. Wakaanza kuwatafuta ngedere. Hawa ngedere ni wanyama wajanja sana. Wanapowaona watu, hujificha juu ya miti. Kwa hiyo waliwatafuta sana mpaka jua likawa kali sana. Baba yake Matiko akasema, "Bora sasa tupumzike chini ya kivuli cha mti huu, tule mabumbunda na kunywa maji. Kila mmoja akala mabumbunda mawili na kunywa maji.

Mara ghafla wakasikia sauti. Wakaacha kula kwanza. Kumbe ilikuwa sauti ya ngedere waliokuwa juu ya mti. Mama ngedere alikuwa akimlisha mwanae.

Waliamka pole pole kuelekea mti wenye ngedere. Walipoukaribia, waliwaona wengine wakicheza karibu. Walikuwa wakiruka kutoka mti hadi mti kwa furaha kama kwamba wanasherehekea jambo fulani. Baba Matiko bila kuchelewa, alifyetua risasi mbili. Yeye alikuwa hodari wa kulenga shabaha kwani alishiriki katika vita kuu ya pili ya dunia. "Phaa, Phaa", mlio wa bunduki uliendelea. na wenziwe waliona ngedere watatu chini ya mti. Wote walikuwa maiti sasa. Waliwachukua nyumbani kuwaonyesha wana kijiji. Waliwachinja ngedere na kuchoma nyama yao. Wanakijiji wengine walileta pombe ya kienyeji na walifanya sherehe kubwa. Walicheza ngoma na kula nyama ya ngedere. Vita baina ya mwanadamu na ngedere iliishia hapo. Matiko alisema, "Sasa tunaweza kutulia, mazao yetu shambani yatakuwa salama mpaka wakati wa kuvuna." Baba yake alimjibu, "Huenda, wengine wakatuingilia tena. Tungoje kwanza kwa majuma machache kama hawata-tokea, basi tutakuwa tumepona."

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu maswali yafuatayo

1. Kuwinda ni kufanya nini?
2. Wawindaji wa hadithi walienda kuwinda wanyama gani? Kwa nini?
3. Matiko na wawindaji wengine walijiandaa je ili kwenda kuwinda?
4. Shamba la familia ya Matiko lilipandwa mazao gani?
5. Kwa nini baba yake Matiko aliweza kuwaua ngedere kwa urahisi?
6. Baada ya kurudi kijijini, walifanya nini?
7. Baba yake Matiko aliamini huu ulikuwa mwisho wa taabu ya ngedere?

Tumia maneneo haya yafuatayo katika sentenzi

mazao	matango	mnyonyaji
kujitegemea	chonga	kivuli
fyetua	chinja	choma

Kazi maalum

Wanafunzi wazungumze juu ya wanyama mbalimbali (i.e. maisha yao, faida zao, hasara zao, na kadhalika).

HABARI ZA SARUFI

A. The -ka- aspect marker

This marker is called an aspect marker rather than a tense marker because it does not have a specific time reference. For example, the past tense which indicates an action done in the past. An aspect infers its time reference from the surrounding time reference. -ka- is used to express a subsequent action or state, a connective idea. It is used mostly in narrated stories (narratives) and follows from a past tense. Therefore, its time reference is inferred from that expressed by the past tense.

It may appear in non narrative sequence as in the following passage:

Najum alikuwa kijana wa Kiarabu wa umri wa miaka ishirini na mitano, lakini nywele zake za kipilipili na pua yake nene ilionyesha waziwazi kuwa yeye ni suriama.

Najum karudi jana kutoka shamba yeye na Bwana Musa.

“Najum was a youth of Arabic ancestry, about twenty five years old, but his kinky hair and thick nose showed that he was clearly a half-cast.

Najum had just returned from the rural area, accompanied by Mr. Musa.”

Mzimu wa Watu wa Kale. M. S. Abdulla (1960:1).

The use of **ka** in **karudi** does not follow from a sequence of action or state. The translation of this sentence does not include a “then” but rather “had just”. However, since the passage is a narrative, **ka** indicates a narrative sequence rather than a sequence of events.

B. The Negative of -ka-

The negative form of a verb with the aspect **ka** is the same as the negative of subjunctives. That is, **si** is used.

For example:

Kwanza alimpiga halafu akampa vitu vyake.

“He beat him up and then gave him his belongings.”

Alimpa kazi halafu asimpe ujira wake.

"He employed him but then he did not pay him."

MSAMIATI

-acha	stop doing something, abandon.
adui	enemy.
-amia	protect a plantation or garden from birds and animals by keeping watch and making noises to scare them away (e.g. scare crow).
-andaa	prepare, set something.
askari	soldier, someone in an army service.
-beba	carry .
-chache	few.
-choma	pierce, insert a sharp object into the body.
-elekea	go/move/ towards, face forward.
-ficha	hide, take cover.
-fyetua	snap, fire (For example: bullets).
-fuka	give out smoke.
ghaffa	suddenly, abruptly, without warning (also used as ghafula).
gogo	log of a tree.
gongo	a thick stick.
hodari	smart, brave.
inchi	inch.
-ingilia	go in for, enter, intrude, pry.
inspekta	inspector.
kali	severe, sharp, hard, bitter.
(ki)enyeji	local native, locally.
kiko	smoking pipe (<i>vuta kiko</i> - smoke a pipe).
-lenga	aim at an object (For example: with a rifle, spear).
(ma)haramia	pirates.
mahindi	corn, maize.
(ma)zao	produce, crop.
maiti	corpse, dead body.
(ma)tango	cucumber.
meta	meter.
(m)janja	clever, cunning.
(mi)koba	handbag(s).
(m)nyonya,ji	sucker, one who lives off others.
(mi)shale	arrows.

msamiati unaendelea

msitu	forest.
mtama	millet.
ngedere	small black monkey.
-kamata	catch, take hold of.
-nyonga	strangle, hang (as in kill by hanging).
-pakia	load onto.
-pakua	unload.
pango	cave.
-panda	plant, grow, (also climb, go up, ascend).
-pora	take by force, steal, plunder, rob.
-pona	survive, escape without hurt, recover from an illness or hardship.
pori	steppe, uninhabited wild land.
-rithi	inherit.
-ridhi	please, content.
-ruka	jump.
rungu	a club curved from wood, mallet.
shabaha	target, aim, intention.
shaka	doubt.
-shiriki	participate.
silaha	weapon.
taabu	hardship, problem, inhibition.
-tulia	settle, be calm, be quiet.
upinde	a bow.
uhandisi	engineering.
-vamia	pounce upon, advance with a rush upon.
vita	war.
-vua	undress, (also catch fish).
-vuna	harvest.
-waka	burn (For example: light, fire).
wevi/wezi	thieves (cf. the singular <i>mwivi/mwizi</i>).
-winda	hunt.

SOMO LA KUMI

MAZOEZI MAALUM

A. Andika sentensi kwa kukanusha au kutokanusha

1. Huyu ni mtoto wake lakini hawakai naye.
2. Mama yake ni mzee sana lakini hawamsaidii hata kidogo.
3. Alinunua viatu vyeusi akampa dada yake kwa sababu havimtoshi.
4. Kuimba kwake ni furaha kwetu.
5. Karatasi hizi zimetoka katika kitabu kile pale.
6. Kama anataka kujenga nyumba, mawe haya hayatoshi hata kidogo.
7. Mpelekee vyombo hivi jikoni.
8. Gazeti la shule hii lina habari nyingi na muhimu.
9. Kutembea kwake usiku, ni tabia yake ya siku nyingi.
10. Kiti kipi kilivunjwa na mtoto huyu?
11. Tulitegemea atarudi jana lakini hajarudi mpaka sasa.
12. Kujua kusoma ni jambo la busara katika ulimwengu wa sasa.
13. Ni adabu mbaya kusema wakati una chakula mdomoni.
14. Mpigie mama yako simu leo usiku.
15. Ni lazima kujifunza mambo haya muhimu ya maisha.

B. Matumizi ya maneno

1. Ukitaka kutafuta maneno haya katika kamusi, utatafuta maneno gani?

yaendelezwe	mazungumzo	akahukumiwa
nitawaambieni	linalofikiriwa	maendeleo;
vijakazi	wanaopendana	mtekelezaji
simtaki	walichotutunukia.	
2. Chagua maneno matano kati ya haya na uonyeshe maana yake kwa kuyatungia sentensi.

Ufahamu

ADUI WA AFYA

Jumanne ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Wazazi wake wanaishi karibu na mji wa Korogwe katika mkoa wa Tanga. Baba yake ni mzee Mweta, ambaye alikuwa na watoto watatu. Kifungua mimba ni Jumanne, na aliyemfuata ni Halima ambaye pia ni mtoto wa kwanza wa kike. Wa tatu ni Bakari. Yeye ni kitinda mimba. Nyumba ya mzee Mweta haikuwa na raha kwa sababu kila mara walikuwa wanaugua na walionekana wadhaifu kutokana na maradhi.

Siku moja Halima akashikwa na homa kali sana. Mwili wake ulikuwa moto, na alikuwa akitetemeka sana. Mzee Mweta hakujuua la kufanya ila kumwita mganga. Mganga alipokuja, alimfunga hirizi shingoni na mkononi. Halima akaona nafuu, lakini kwa bahati mbaya baada ya siku tatu akafariki. Huzuni na hofu ikazidi sana nyumbani mwa mzee Mweta.

Kila wakati Jumanne alipokuwa nyumbani kwa likizo alikuwa akipendelea sana kukaa na baba yake na kuzungumza juu ya mambo mbali mbali. Baba yake alimwambia kuwa marafiki zake wamemliwaza juu ya kifo cha Halima. Walisema kuwa yote yaliyotokea ni amri ya Mungu. Alikiri kwamba hakuamini maneno haya.

Miezi mitatu baada ya kifo cha Halima, Bakari alishikwa na ugonjwa wa kuhara. Wakati huo, mama yake Bakari alikuwa Mbozi akimwuguza shangazi yake aliyekuwa mgonjwa mahututi. Mzee Mweta alianza kuwa na wasiwasi. Kwa bahati nzuri, jirani yao ndugu Hiza ambaye alikuwa daktari wa hospitali ya Mheza alikuwa nyumbani kwa likizo.

Mzee Mweta aliyakumbuka maneno ya mwanae Jumanne alipokuwa nyumbani mara ya mwisho. "Baba, magonjwa kama haya yamewasumbua watu wengi hapa nchini. Magonjwa haya yanaletwa na maji machafu, hayawezi kutibiwa kwa uganga wa kienyeji. Ni budi kwenda kuonana na daktari, na sio mganga, mara dalili ndogo zionekana."

Mzee Mweta alimchukua mwanae Bakari na kumpeleka nyumbani kwa daktari Hiza. Alikuwa na hofu sana. Aliamua kwenda kumwona daktari Hiza, ili mwanae Bakari asije akamfia kama Halima alivyomfia. Daktari Hiza alimchunguza mgonjwa na kukata shauri wampeleke hospitali mara moja. Daktari Hiza aliwachukua katika gari lake mpaka hospitali ya Mheza. Bakari aliandikiwa kitanda (yaani alilazwa hospitalini) ili uchunguzi uanze

kufanywa na apatiwe matibabu yafaayo. Kwa sababu daktari Hiza alikuwa jirani yao, alianza kumshauri juu ya adui wa afya. Alimshauri juu ya mbu wa malaria, na nzi waletao magonjwa mbali mbali kutokana na uchafu. Aliwashauri pia kuepuka kunywa maji ambayo hayajachemshwa, na pia wayaweke maji hayo katika vyombo vifaavyo, na pia safi.

Mzee Mweta alikiri kwamba mwanae Jumanne alikwisha kumshauri hivyo pia, na wameanza kujitahidi kujenga nyumba safi, choo, na bafu la kuogea. Alisema mwanae Jumanne amalizapo masomo yake ya Chuo Kikuu atakuwa Bwana Afya na ataleta huduma hizo nyumbani. Alitegemea pia kwamba kipato cha mwanae baada ya kuajiriwa na serikali kitakuwa kinawasaidia kuendeleza na kuinua maisha yao. Wataweza kula vizuri zaidi na kulala vizuri. Maadui wa afya hawataweza kuwapata kamwe. Alikiri kwamba, watu wathaminio usafi na wafuatao kanuni za afya hawana taabu nyingi za afya.

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu maswali yafuatayo

1. Maadui wa afya ni nani?
2. Ugonjwa gani uliomwua Halima?
3. Bakari alikuwa na ugonjwa gani?
4. Nini tofauti baina ya matibabu aliyopewa Bakari na yale aliyopewa dada yake?
5. Daktari Hiza alimshauri nini Mzee Mweta?
6. Mzee Mweta alikuwa na mategemeo gani ya baadaye kuhusu afya bora nyumbani kwake?

Msamiati: Chagua neno au kifungu cha maneno kutoka B ambalo lina maana sawa na neno au kifungu cha maneno katika A

A.

- | | | | |
|-----|------------------|-----|---------------|
| 1. | kifungua mimba | 2. | kitinda mimba |
| 3. | maradhi | 4. | udhaifu |
| 5. | huzuni | 6. | nafuu |
| 7. | likizo | 8. | kufa |
| 9. | epuka | 10. | jitahidi |
| 11. | andikiwa kitanda | 12. | kamwe |
| 13. | chooni | 14. | uchunguzi |

B.

- | | | |
|-----------------|-----------------|-----------|
| mtoto wa mwisho | afadhali | utafiti |
| msalani | lazwa hospitali | magonjwa |
| jaribu | fariki | jihadhari |
| kabisa | mapumziko | uchungu |
| unyonge | mtoto wa 'wanza | |

Kazi Maalum

Wanafunzi wazungumze juu ya magonjwa yanayowasumbua watu katika sehemu waishizo.

HABARI ZA SARUFI

A. More on negatives

1. The negative form of the infinitive form marked by *ku* is *kuto* which is a remnant of *kutoa* "to remove", "to give away", "to subtract." Thus: *kuimba* → *kutoimba*.
2. The negative form of the subjunctive is *si*. This form appears after the subject prefix. The final vowel remains as *e*. For example: *tukawie* → *tusikawie*.

B. Compound tenses

Compound tenses can be of the same type as in:

- a. **Mganga alipokuja alimfunga hirizi shingoni.**

Notice that the two verbs have identical tense markers *li*. In such cases the speaker wants to express an action which is resultant or consequential

to the preceding one. When different tenses are used, it indicates different aspects of the actions involved. Generally an auxiliary verb is used and the most common are **kuwa**, **kuja**, and **taka** as in:

- b. **Alikuwa anasoma.** (tense + tense)
"He was reading."
- c. **Atakuwa akiwapikia watoto utakapofika.** (tense + aspect)
"She will be cooking for the children when you come."
- d. **Usiwe unanisumbua kama unaona mlango umefungwa.** (subjunctive + tense)
"Do not disturb me if you see the door is closed."
- e. **Alikuwa na hofu Bakari asiye akamfia kama Adija.** (subjunctive + aspect)
"He was afraid that Bakari might die on him like Hadija did."
- f. **Wamekuwa wanatusaidia kwa miaka kumi sasa.** (aspect + tense)
"They have been helping us for ten years now."

The auxiliary verb expresses one aspect of what is being expressed while the main verb expresses the other aspect (cf. Lesson 19 for a discussion of the function of each auxiliary verb.)

The **-ki-** tense is interesting because it can be used interchangeably with **-na-**. It is used to express a continuous or repetitive action. Thus in (b) above the **-na-** can be replaced by **-ki-** and in (c) the **-ki-** can be replaced by **-na-**. The ability to substitute for **-na-** has made **-ki-** to be considered a simple tense. In Lesson 11 we will discuss other functions of **-ki-** in compound tense.

MSAMIATI

dalili	sign.
-chinja	slaughter, cut the throat of, kill animals for food.
choo	privy, cesspit, movement of the bowels.
-epuka	avoid.
-fariki	die(esp. of natural cause).
-hara	have diarrhoea.
hirizi	charm, amulet.
hofu	fear.
-inua	lift, uplift.
-jaribu	try.
-jenga	build, construct.
-jihadhari	take precaution, make safe.
kamwe	not/ at all, once, in the least, ever; by no means.
kanuni	conditions, rules, fundamentals.
-kawia	delay in returning, overstay.
kifungua mimba	first born.
kipato	earnings, income, salary.
-kiri	admit, agree.
kitinda mimba	last born.
kulazwa	to be admitted in hospital (also <i>kuandikiwa kitanda</i>).
likizo	holiday, vacation, resting period, leave of absence.
-liwaza	comfort, soothe, quieten.
(ma)azimio	intention, scheme, program of work.
(ma)endeleo	progress, development.
mahututi	critical condition in an illness.
(ma)pumziko	rest, resting period.
maradhi	sickness, illness, disease.
matibabu	cure.
msalani	bathroom, lavatory.
nafuu	improve, make progress, convalescence.
nzi	house fly.
-thamini	put value, respect.
udhaifu	body weakness.
uchungu	bitterness, pain.
uchunguzi	investigation, research, looking into something.
-ujenzi	construction, act of building.
unyonge	wretchedness, weakness, abject, destitution.
utafiti	research.
wasiwasi	anxiety.

SOMO LA KUMI NA MOJA

MAZOEZI MAALUM

A. Jaza nafasi hizi kwa kutumia vipengele vifuatavyo

-cho-, -u-, -ya-, -pa-, -ku-, -ji-, a-, -ku-, -ni-, -ki-.

1. Ali.....umiza kidole, na sasamefunga kitambaa.
2. Nita.....vunja mkono kama uta.....chezea.
3. Ume.....ona kitabu chako kili.....potea.
4. Siku.....fungua mlango lakini nili.....fungua madirisha.
5. Si.....jui anapokaa, bali nina.....jua anakofanya kazi.

B. Tafsiri kwa Kiingereza

1. Chakula hiki kingepikwa vizuri, kingeliwa chote.
2. Kama mti huu ungekatwa mapema, ungefaa kwa kuni wakati wa masika.
3. Kama unataka kumtembelea, mpigie simu au mwandikie barua.
4. Ukimwona, mwambie ninamtafuta.
5. Kama ukitaka kuwa mwanasheria hodari, budi ujifunze kutetea haki za wateja wako.
6. Kweli hukumtafuta meneja wa kijiji. Ungalimtafuta, ungalimkuta na wanakijiji shambani, akilima.
7. Iwapo utahitaji msaada, usisite kunijia.
8. Ikiwa una pesa za kutosha, hakuna sababu kwa nini usiende Afrika.
9. Ungalimwona, ungemwambia nini?
10. Akitaka kupanda mlima Kilimanjaro atahitaji vifaa gani?

Ufahamu

MCHEZO WA NG'OMBE

Mimi si mwana-michezo, lakini huifurahia michezo inapochezwa. Miongoni mwa michezo mingi niliyokwisha kuiona, hakuna ulionivutia zaidi kuliko mchezo wa ng'ombe. Niliuona mchezo huu nilipotembelea Pemba miaka michache iliyopita. Ninge kuwa na uwezo ningejifunza kuucheza mchezo huu.

Mchezo wa ng'ombe unajulikana sana na wenyeji wa Pemba. Ni mchezo waupendao mno wenyeji wa Pemba. Vitabu vya Historia vya eleza kwamba,

asili ya mchezo wa ng'ombe ni Ureno. Ajabu iliyopo ni kule mchezo wa ng'ombe kufika Pemba na mahali ambapo ni mbali mno kutoka Ureno. Ingawa tunajua kwamba Wareno waliwahi kuzitawala pande hizi katika karne ya 16 na 17, vitabu hivi vingaliandikwa na mtu wa Pemba, vingalituambia kuwa chanzo cha mchezo huu ni hapa hapa Pemba.

Mchezo huu unaendelea kucheza hapa Pemba na huwavuta watu wa kila aina. Kama uwanja wa michezo usingekuwa mkubwa ya kutosha, watu wengi hawangeweza kuingia kuuona mchezo huu uchezwapo. Siku hizi kama mtu akitaka kupata nafasi nzuri sharti awahi kiwanjani masaa mawili au matatu kabla ya mchezo kuanza.

nanga	anchor (<i>tia nanga</i> = to anchor).
-nasihi/-sihi	give good advice, to counsel wisely.
-ngara	shine, light up.
ng'oa	root up, pull up, dig out.
-nong'ona	whisper.
-nyamaa/nyamaza	be quiet, stop talking/crying/shouting.
-pepea	fly, wave about in the air, blow up with wind.
-randa	move from one place to another aimlessly.
Ras/rasi	cape, head, chief.
-rejea	arrive, come back, return.
-sindikiza	escort, accompany.

msamiati unaendelea

staha

suala/swala/swali

-tahamaki

-tulizana

ustahimilivu

ukucha

utulivu

respect, honour, reverence.

question, inquiry, something for consideration.
look up suddenly, observe instantly.

calm down, be calm/quiet, be composed.
endurance, patience.

finger/toe nail.

calmness, peacefulness, quietness, gentleness.
(-tulia be calm, composed, be quiet)



SOMO LA KUMI NA SABA

MAZOEZI MAALUM

A. Ziandike upya sentenzi zifuatazo ukizianza kwa kutumia maneno yaliyowekwa katika alama za vifungo ()

1. Susana alimpiga dada mgongoni kwa fimbo (dada).
2. Sefu amempeleka Rajabu hospitali (Rajabu).
3. Nilipomtikisa, alianza kulia (yeye).
4. Babu alimwua ng'ombe kwa urahisi sana (ng'ombe).
5. Tajiri alimdhulumu maskini mali yake yote (maskini).
6. Alizitupa pesa zote alipoona wanyang'anyi wanamkaribia (pesa)
7. Alimpa mama yake mizigo aliyoleta (mama yake).
8. Niliwaambia wanawake wale waende nyumbani(wanawake).
9. Uledi aliunyanyua mzigo mzito (mzigo mzito).
10. Nyamaume waliwashika makuli (makuli).

B. Chagua neno lifaalo kujaza nafasi iliyoachwa katika kifungu hiki ili hadithi ilete maana kamili

magofu	gungu	daraja
Serikali	ilifukuliwa	ndipo
hayajachunguliwa	Maganjo	Waswahili
kale	yanalindwa	sherehe
yenye	kaburi	wenyeji.

Pengine wengi wetu hawajui kuwa mahali ilipo shule kubwa ya Mombasa hivi leo, karibu na linalokiunga kisiwa hicho na bara la Afrika kiini cha mji wa wa Mombasa. Ilipojengwa shule hii mwaka 1919, yalivunjwa na mifupa mingi ya wanadamu

Leo limebaki la Shehe Mvita na makaburi mengine ya zamani, na magofu ya misikiti na majumba mengine. Kila mwaka wa asili wa Mvita huja kulizuru kaburi la Shehe Mvita na hapo hufanya zao za "Siku ya Mwaka" kwa hesabu ya Hapo huchinja ng'ombe na kucheza ngoma inayoitwa yenyewe sana ijapokuwa katika sheria. ya Kenya inajaribu sana kuhifadhi mambo kama haya.

ELIMU YA KUJITEGEMEA

Elimu ya kujitegemea si jambo geni kwa nchi nyingi za Kiafrika. Watoto walifunzwa na wazazi wao kujitegemea wangali watoto. Mara mtoto apatapo fahamu ya kujua mambo yanayomzunguka, wazazi walijaribu kidogo kidogo kumzoesha kufanya mambo machache huku wakimwongoza pole pole. Kwa mfano mtoto wa umri wa miaka mitatu alianza kujifunza kunawa mikono na kurudisha chombo alicholia chakula kwa mama. Apatapo umri wa miaka minne, huanza kwenda mtoni na kaka au dada zake na kuanza kujifunza kuchota maji. Maji haya huyatumia kwa shughuli zake za kucheza au mara nyingine kwa akili zake mwenyewe humpa mama yake na kumtaka ampikie chakula kwa kutumia maji haya.

Kadri anavyokua, mtoto hujifunza kuvaa nguo na kuweka vitu vyake katika hali ya usafi. Watoto wengi huanza kujifanyia shughuli zao binafsi kama kulima bustani ndogo, kufuga kuku au wanyama wengine wadogo. Hutumia mapato wapatayo kwa kujitimizia haja zao pale ambapo wazazi hawawezi kuwapa kila kitu. Kwa namna hii, huwa watu wazima wakijua kwamba kazi ni muhimu na kwamba kujitegemea ni jadi ya Mwafrika.

Katika shule za Tanzania, elimu ya kujitegemea inahimizwa sana. Wanafunzi wanategemewa kujifunza masomo ya nadharia na kutumia nadharia hiyo katika kuendeleza shughuli mbalimbali za kilimo, ufundi, ufugaji na kadhalika. Nia ya serikali ni kuwaelimisha wananchi kutambua kwamba elimu itolewayo ina madhumuni ya kuwaandaa vijana kulitumikia taifa lao, na sio kutimiza haja ya kuingiza desturi za kigeni ambazo haziendani na mila na desturi za Mwafrika.

Mfumo wa elimu iliyoenezwa na nchi zilizotawala Afrika wakati wa ukoloni ulikuwa na lengo la kutayarisha makarani na maofisa wa vyeo vya chini. Kutokana na mabadiliko ya elimu baada ya uhuru, nchi nyingi zimeanza kuwaandaa vijana wake kushika nafasi zote muhimu za kazi katika serikali, katika mashamba, na katika viwanda. Kwa hivyo, ni budi wananchi waelewe misingi ya elimu ya kujitegemea ambapo mawazo ya ubwana na utwana hayapo. Kila mwananchi sharti ajue kwamba kufanikiwa kwake au kwa taifa zima kunategemewa juhudi za kila mwananchi kujua kujitegemea.

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu Maswali haya

1. Kwa nini mwandishi anasema “elimu ya kujitegemea si jambo geni”?
2. Katika maisha ya mtoto wa Kiafrika, ilidhihirikaje kuwa anajifunza kujitegemea?
3. Elimu ya kujitegemea inawekewaje mkazo katika shule za Tanzania?
4. Nini tofauti baina ya elimu ya mfumo wa kikoloni na elimu ya sasa katika nchi nyingi za Kiafrika.

Andika sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo

shabaha	haja	desturi
makarani	mfumo	imani
andaa	wanyonge	juhudi

Kazi Maalum

Wanafunzi wjadiliane juu ya mada ya “kujitegemea”



MSAMIATI

-andaa	prepare, get ready.
desturi	custom, usage, regular practice, routine.
-dhihirika	become clear, obvious.
-dhulumu	treat unjustly, defraud, oppress.
-eneza	spread, cause to be widely known.
-fukia	cover with soil, fill a hole with soil.
-fukua	uncover, unearth, dig out.
geni	foreign, new.
gungu	a mode of dancing.
haja	need, urge, requirement.
-hifadhi	reserve, protect, put in sanctuary.
-ingiza	make enter, insert.
jadi	pedigree, genealogy, ancestry, descent.
-jadili(ana)	discuss (with each other).
juhudi	effort.
-karibia	get close, approach.
maganjo	deserted village or town, ruins.
(ma)gofu	ruins, emanciated, broken down.
(m)fumo	a way things are, connectedness of things, process.
(m)sikiti	mosque.
(m)zigo	load.
mila	custom, habit, propensity.
nadharia	theory.
-nawa	wash oneself lightly.
shabaha	target, aim, intention, ambition.
sheria	law, regulation, code of conduct.
-tikisa	shake violently, cause a vibration.
-timizia	fulfill, accomplish, finish.
ufundi	technical ability.
-vunja	break.
(vy)eo	rank(s).
(wa)nyang'anyi	robbers.
-zoesha	cause to get used to something, acquaint.
-zunguka	circle around, wander around.

SOMO LA KUMI NA NANE

MAZOEZI MAALUM

A. Badilisha sentensi hizi kwa kutumia usemi wa msemaji

1. Juma alisema anaenda nyumbani.
2. Yohana alisema kwamba alichapwa fimbo kumi.
3. Aliniuliza kama nina taabu gani.
4. Wazee wake walisema kwamba wanapenda kusafiri.
5. Alisema kwamba Mwanæ aliugua homa ya malaria.
6. Alinisih niweke pesa zangu zote benki ili kujiepusha na wizi.
7. Alisema kuwa watoto wajanja wanazaliwa wajanja.
8. Alitambia tufanye zoezi la nyumbani.
9. Jemadari aliwaambia askari wake waendele mpaka wawakabili maadui.
10. Aliniuliza vile ningefanya kama ningekuwa nduguye.

B. Andika tarakimu hizi kwa maneno

- | | |
|------------------|-------------------|
| 1. $\frac{1}{2}$ | 6. $\frac{3}{8}$ |
| 2. $\frac{1}{4}$ | 7. $\frac{5}{6}$ |
| 3. $\frac{3}{4}$ | 8. $\frac{1}{3}$ |
| 4. $\frac{2}{5}$ | 9. $\frac{1}{6}$ |
| 5. $\frac{2}{3}$ | 10. $\frac{2}{6}$ |

Ufahamu

CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM


Miaka michache iliyopita wengi tusingesadiki kwamba watoto wetu wange-weza kupata shahada kutoka chuo chetu wenyewe. Kutokana na mfumo wa elimu uliowekwa kabla ya uhuru, watu walikuwa wakifikiri kwamba kupata masomo ya juu ni lazima kwenda Ulaya au Amerika. Kwa sababu hizi hata vyuo vyetu vilipoanza humu Afrika, wengi walikuwa hawaridhiki kwamba vijana wanapata masomo ya kweli walipoingia vyuo hivyo. Wakati

huo umepita na nchi nyingi za Kiafrika sasa zina vyuo ambavyo ni kama mwanga ambao lazima umulike pote pote Afrika na kusaidia kujenga Afrika nzima.

Tanzania ina vyuo vikuu viwili sasa. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambacho kiko mjini Dar es Salaam, na Chuo Kikuu cha Sokoine ambacho kiko mjini Morogoro.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ndicho kilichokuwa chuo kikuu cha kwanza Tanzania. Chuo hiki kiko karibu na mji, mahali ambapo zamani palikuwa hakuna majengo lakini ambapo sasa kumezuka viwanda vya kila namna karibu nacho. Sehemu za Ubungo si pori tena, ni nyota ya maendeleo baada ya Uhuru.

Wazo la kuanzisha Chuo Kikuu katika nchi ya Tanganyika (kama ilivy- ofahamika wakati huo), lilitolewa kwa mara ya kwanza katika ripoti ya "Elimu ya Juu" kwa nchi za Afrika ya Mashariki mnamo mwaka 1955. Kutokana na ripoti hiyo, Chuo Kikuu kilitazamiwa kujengwa nchini Tanganyika, baada ya miaka kumi kuisha. Lakini jambo hili lilitiwa nguvu na kuharakishwa, wakati chama kitukufu cha TANU nchini Tanganyika kilipo- jipatia madaraka ya kutosha serikalini. Mnamo mwaka 1961, mwezi Febru- ari, hati ya muda ya Halmashauri ya Chuo Kikuu ilipitishwa katika Bunge, na hivyo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kikaanzishwa.



Wakati wa mwanzo shughuli zote za Chuo hiki ilibidi ziendeshe kwenye majengo ya muda. TANU ilikubali jengo lake lililokuwa mtaa wa Lumumba mjini Dar es Salaam likodishwa kwa ajili ya shughuli za Chuo Kikuu. Lakini jinsi Chuo kilivyozidi kukua ilibidi kukodisha majengo na mabweni ya muda kwa ajili ya wanafunzi wa kwanza. Majengo yaliyokodishwa yalikuwa Msimbazi na kwenye kambi za Jeshi la Wokovu Mgulani.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilifunguliwa rasmi na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (wakati huo akiwa Waziri Mkuu wa Tanganyika na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Afrika ya Mashariki) mnamo tarehe 25 Oktoba, 1961. Wakati huo kilikuwa na wanafunzi kumi na nne tu walioanza mafunzo ya Uanasheria. Mnamo mwezi Julai mwaka 1963 idadi ya wanafunzi ilikuwa themanini, thelathini na watano kutoka Tanganyika, ishirini na moja kutoka Kenya na ishirini na wawili kutoka Uganda, mmoja kutoka Malawi, na mmoja kutoka Zambia. Mkuu wa Chuo wa kwanza alikuwa Bwana R. C. Pratt, na naibu wake alikuwa Dr. W. K. Chagula ambaye alikuwa Mkuu wa Chuo Msajili. Dr. Chagula alikuwa Mkuu wa Chuo baada ya Bwana Pratt. Nafasi ya Dr. Chagula kama Mkuu wa Chuo Msajili ilichukuliwa na Ndugu G. R. Kunambi.

Ilikuwa mnamo mwezi wa Juni mwaka 1964 wakati Chuo Kikuu kilipo-
hamia vkwenye majengo mapya na ya kudumu yaliyoko sehemu iliyoitwa wakati huo 'Observation Hill' na ambayo sasa inaitwa 'Mlimani'. Sehemu hii ni umbali wa maili nne hivi kutoka mjini. Tangu hapo, majengo yamezidi kuongezeka kulingana na kupanuka kwa shughuli za Chuo Kikuu.

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu Maswali yafuatayo

1. Kutokana na mafunzo ya kikoloni, watu walifikiri ni lazima mtu afanye nini ili apate masomo ya juu?
2. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni kama nini kwa wananchi wa Tanzania?
3. Wazo la kuanzisha chuo Kikuu lilitolewa wapi na lini?
4. Shughuli za mwanzo za Chuo Kikuu ziliendesha wapi?
5. Mwanzoni kulikuwa na wanafunzi wangapi? Walitoka wapi?
6. Aliyekuwa Mkuu wa Chuo Msajili wa kwanza ni nani? Alikuwa mkuu wa Chuo lini?
7. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam bado kiko katika majengo ya muda?

Kujenga Msamiati

Nini maana ya maneno haya. Unaweza kutunga sentenzi kama nja mojawapo ya kuonyesha maana ya maneno haya.

-sadiki	shahada	-ridhika
-zuka	-kodisha	madaraka
-mulika	pori	hati
shughuli	naibu	-hamia

Kazi Maalum

Wanafunzi wafanye utafiti juu ya historia ya chuo au shule waliyosoma na kutoa taarifa hiyo darasani.

HABARI ZA SARUFI

Direct speech is characterized by quotation marks (*"hujambo"*). Reported speech is characterized by either of the following conjunctions: *(ya) kwamba, (ya) kuwa, (ya) kama*. It may also be introduced by any of the following verbs:

ambia.... in reporting a statement made by one person to another.

sema.... in reporting a general statement.

uliza.... in reporting a question.

taka/amua 'decide'....in reporting a decision, intention, or an order.

Mifano

1. "Nendeni nyumbani tafadhali", mwalimu aliwaambia.
Mwalimu aliwaambia waende nyumbani.
2. "Tunataka kuwaona watoto wetu", wazazi walisema.
Wazazi walisema (kwamba) wanataka kuwaona watoto wao.
3. "Mnataka kwenda wapi?", aliuliza.
Alituuliza (kama) tunataka kwenda wapi.
4. "Njoo hapa sasa hivi", mwalimu alisema.
Mwalimu alitutaka tuende pale wakati ule.
5. "Nitaondoka kesho bila kukosa", alisema kwa hasira.
Aliamua kwamba ataondoka kesho bila kukosa.

B. Fractions

The following are useful fractions.

- $\frac{1}{2}$ = nusu.
 $\frac{1}{4}$ = robo.
 $\frac{3}{4}$ = robo tatu au moja kasoro robo.
 $\frac{1}{3}$ = theluthi moja.
 $\frac{2}{3}$ = theluthi mbili.
 $\frac{1}{5}$ = moja ya tano.
 $\frac{1}{6}$ = sudusu.
 $\frac{1}{8}$ = thumni moja.

MSAMIATI

bunge	house of parliament.
chama	union, an organisation, a party with a political stand.
hamia	migrate, move to a new location.
hati	certificate.
idadi	amount, a measure which involve numbers.
jeshi	army, military army.
-kabili	confront, overcome, endure.
-kodisha	rent, lease.
(ma)daraka	power, government.
msajili	registrar.
-mulika	throw a beam of light on an object, gleam.
(m)wanga	light.
naibu	deputy, one who can take up duties of his superior.
-ridhika	be satisfied, contented.
ripoti	report.
-sadiki	believe, have confidence.
shahada	degree, a certificate of academic achievement.
-tazamiwa	expect, look forward to.
tukufu	honorable, supreme.
uanasheria	pertaining to law.
umbali	a measure of distance.
(wa)janja	clever, cunning.
wokovu	salvation.

SOMO LA KUMI NA TISA

MAZOEZI MAALUM

A. Ziandike sentensi zifuatazo kwa kuzianza kwa maneno katika vifungo ()

mfano: Alipikiwa chakula cha mchana na mama.

Mama alimpikia chakula cha mchana.

1. Aliambiwa aende mtoni mara tano na mama.
2. Amepewa fedha za kumtoshia kwa safari yake na baba.
3. Waliulizwa habari za nyumbani na shangazi.
4. Utapelekwa mahakamani kama utakamatwa na askari.
5. Askari wote wamejeruhiwa vibaya na adui.
6. Alikamatwa akitangatanga mjini bila kazi na polisi.

B. Andika sentensi zifuatazo ukitumia maneno katika vifungo bila kugeuza maana ya sentensi

1. Nilifika mapema lakini sikumkuta (ingawa).
2. Alikimbia sana mpaka akapata zawadi (kwa sababu)
3. Sababu ya kufanya hivi ni kuonyesha desturi za kabila (ili).
4. Mtoto aliyemwa na nyoka yuko hospitalini (amba.....)
5. Waliondoka wakaenda kwingine (mahali).
6. Watoto wamerudi katika darasa (darasani).
7. Asingeiba asingefungwa jela (kama).
8. Sikumkuta baba na sikumkuta mama (wala).
9. Chumba hiki si kibaya hata kidogo (kizuri).
10. Aliweka maziwa ndani ya kabati (kabatini).

Ufahamu

KUCHAGUA MCHUMBA KWA WACHAGA

Katika jamii ya Wachaga, wavulana na wasichana huachwa huru kujichagulia wachumba wao, bila maingilio ya wazazi wao. Tangu utoto, watoto wa kiume na wa kike hukutana na kuzungumza mara nyingi hata wakaweza kujuana sana kabla ya kuanza kuchumbiana. Kwa hivyo hakuna haraka katika kujichagulia mke au mume.

Mvulana anapojisikia anampenda msichana fulani, hawezi kumwambia msichana mwenyewe kuwa anampenda mbele ya watu. Kama anafanya hivyo, itafikiwa kuwa ni utovu wa adabu na kutojua mila na desturi za kabila. Kwa hivyo mvulana humwambia rafiki mmoja au wawili katika hirimu yake. Hapo wote huenda kumtembelea huyo msichana. Wakishafika nyumbani kwa msichana, huingia ndani ya nyumba ya mama yake. Msichana na mama husalimiana na wavulana hawa halafu mama huwapa viburudisho. Baadaye, mama hutoka na kwenda zake kuwaachia watoto hawa nafasi ya kuzungumza. Mmoja wa wavulana anaweza kumwuliza msichana kama anataka kufahamu kwa nini wamemtembelea. Msichana hujibu kama si lazima kwa sababu kwa desturi ya Wachaga, kila apitaye njia anaweza kukaribishwa kula na jamaa. Basi, hapo mvulana mmoja anamwambia kuwa wanatafuta makao ambako wanaweza kupokelewa na kupewa chakula na ulinzi kila wakati na sio kama wapita njia. Kwa maneno mengine wanataka kuwa watoto wa nyumba hiyo. Kwa tamko hilo, msichana hujua mara moja nia yao. Basi huwauliza kusema wazi wazi ni nani kati yao anayetaka kuwa mwenyeji wa nyumba yao. Hapo mvulana mmoja humtambulisha anayekusudia kumtaka uchumba msichana huyo. Ikiwa atamtaka awe mumewe, huwaambia waende zao na kurudi siku nyingine. Wakati mwingine matembezi kama hayo hufanywa mara mbili au tatu hivi. Wakati anapotoa jibu la mwisho, msichana huwaambia, "Nakubali mwana wa Fulani apokelewe katika ukoo wetu.

Sherehe zote za arusi hufanywa na baba na mama wa mvulana. Kwa hivyo, mvulana hushauriwa azungumze na wazazi wa msichana juu ya mipango ya arusi. Ikiwa wazazi wa msichana watamkubalia mvulana, basi shughuli za arusi huanza.

Kama msichana hampendi mvulana huyo, husema, "Nyumba yetu si kubwa ya kutosha kwa mtu mwingine wakati huu." Jibu hili huwatahadharisha wavulana kuwa wamekataliwa. Wataondoka kwa huzuni, lakini hawatakuwa na chuki juu ya familia hiyo.

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu maswali haya

1. Mchumba huchaguliwa na nani?
2. Orodhesha hatua achukuazo kijana kama amampenda msichana fulani.
3. Sherehe za arusi hufanywa na nani?
4. Msichana hutumia usemi gani iwapo hapendi kuolewa na kijana fulani? Nini maana kamili ya usemi huo?

Kazi Maalum

Wanafunzi wajadiliane juu ya mila na desturi maalum katika jamii yao.

HABARI ZA SARUFI

Auxiliary Verbs

We made mention of some of the auxiliary verbs in Lesson 10. These are **kuwa**, **kuja** and **-taka**. Others are **-enda** and **-weza**. They are considered auxiliary verbs when they appear with another verb which contains the main information of an event. The auxiliary verbs carry additional information which is crucial to the information in the main verb.

1. **kuwa** is used to indicate a static situation. As we noted in Lesson 10, the main verb may express a continuous action if the progressive aspect marker **-ki-** or the tense **na** are used. For example:

Alikuwa akisoma.

Alikuwa anasoma.

"He was reading."

The presence of the verb **kuwa** makes the verb **soma** express a static situation. The static situation will bear a time reference which is expressed in the verb **wa**. In the examples above, the time reference is **past** and it is expressed by **li**. Any of the other tense and aspect markers may likewise be used.

2. **-enda** may be used as an auxiliary verb. It may co-occur with any of the tense or aspect markers to indicate the time of the action of the main verb. The main verb is expressed in the infinitive form. For example:

Alienda kutembea.

"He went to walk."

When used with a relative of time **-po-** with or without the subject prefix, it indicates probability.

For example:

Endapo atafika, tutafanya uamuzi kamili.

"Should he come, we will then make a definite decision."

Endapo may also be used instead of **ikiwa**, **kama** (cf. Lesson 12) to express a condition.

Huenda 'may be' can also be used as an auxiliary verb and when it combines with any tense or aspect marker, it will express probability. Further, when it is used with tense markers, it will imply that the proposition is highly probable. Otherwise, when used with aspect markers like **ka**, it will imply that the proposition is less probable.

For example:

Huenda akaja leo.

"May be he will come today/He might come today."

3. As an auxiliary verb, **-weza** expresses ability, potentiality or possibility. The main verb is expressed in the infinitive except in conditionals.

For example:

Anaweza kusoma hapa.

"He can study here."

Akiweza atakusaidia.

"If he can he will help you."

Angeweza angekusaidia

"If he could he would help you."

4. Another auxiliary verb, **-taka** is used to indicate a "point of departure". Like in the other cases with auxiliary verbs, the main verb is expressed in the infinitive.

For example:

Alitaka kutembea tu.

"He just wanted to walk."

MSAMIATI

-acha arusi chuki -chumbia hirimu huzuni -jeruhi -kataa -kubali -kusudia mahakama (ma)ingilio (ma)tembezi (m)chumba mila (mi)pango orodha sherehe -tahadhari(sha) tamko -tangatanga ulinzi ukoo utovu usemi wazi wazi	leave, cease, stop an on-going action. wedding. anger, bitterness, rage. courting. age period of life (between 10-25), contemporary. sadness, unhappiness, bad feeling. injure. refuse, deny. agree, accept, acknowledge. intend, plan to. court house. intrusions, interventions. a walk, a stroll, a visit. fiancé. traditions, culture. arrangement, plan, organization. a list. celebration, feast. be cautious, avoid, be on guard (against). announcement, statement, pronouncement. wander around, be without a specific place of abode. security. clan, familyhood, of the same ancestry. misconduct. a way of talking, pronouncement, a say. clearly, plainly.
--	--

SOMO LA ISHIRINI

MAZOEZI MAALUM

A. Weka vituo na herufi kubwa pafaapo

mwalimu mkuu alitoka nje na kusema nitelee vitabu vyangu tafadhali mwanafunzi aliingia ofisini kwa mwalimu na kumletea vitabu hivyo mara ghafula wakaona motokaa ya mkuu wa elimu inaingia mwalimu mkuu aliondoka mara kumpokea mkuu wa elimu wanafunzi walisimama kwa adabu na kumwamkia mkuu wa elimu yeye alisema nina habari njema kwenu shule yenu imechaguliwa kushiriki katika mashindano ya kitaifa ya elimu ya kujitegemea serikali itatoa shilingi elfu tano kama msaada kwenu ili muweze kushiriki kikamilifu wanafunzi na mwalimu walifurahi sana na walimshukuru mkuu wa elimu baada ya kuondoka mwalimu pamoja na wanafunzi walianza mazungumzo juu ya matayarisho ya mashindano haya

B. Tumia maneno yafuatayo ili kukamilisha sentenzi hizi (unaweza kutumia neno zaidi ya mara moja)

ona, meza, ua, jambo, jua.

1. Unaweza kuugua kama uta..... chakula bila kukitafuna.
2. Ninataka kukaa juani kwa sababu nina..... baridi sana.
3. Alipofika hapa haku..... mtu ye yote.
4. Vitabu vyangu viko juu ya
5. Kumwibia mtu mali yake ni linalostahili adhabu kubwa.
6. Aliweka nguo zake juu ya ulioizunguka nyumba yake.
7. Tulipokutana naye alisema ham..... ?
8. Hapa Marikani, ni kali sana mwezi Julai na Agosti.
9. hili linaitwa waridi.
10. Alisema kwamba ana..... mahali anapokaa.
11. Simba aliwa..... twiga wawili.

Ufahamu

UTEUZI WA LUGHA YA TAIFA

Lugha ya taifa ni ile ambayo imeteuliwa kwa matumizi ya wananchi wote. Kwa kawaida, lugha hiyo huzuliwa katika lugha nyingi zinazozungumzwa nchini. Kwa mfano, huko Tanzania kuna lugha zaidi ya mia moja, lakini Kiswahili kiliteuliwa kuwa lugha ya taifa.

Ni nchi chache sana ulimwenguni ambazo hazikuwa na shida ya kuunda lugha ya taifa. Ingawa ni fahari kubwa kwa nchi kuwa na lugha yake ya taifa, si rahisi jambo hilo kufanyika.

Moja kati ya tatizo kubwa la nchi zinazoendelea, nchi ambazo kwa miaka nenda na miaka rudi, zimekuwa chini ya utawala wa kikoloni, ni kule kujiamulia ipi kati ya lugha zake iwe lugha ya taifa. Ni tatizo kubwa sana na pengine hata kushinda tatizo la uchumi. Tatizo hili sio la nchi changa tu, bali ziko nchi zilizoendelea, kwa mfano Ubelgiji, na Uswisi ambazo zinatumia lugha za jirani zao kama lugha rasmi kwa sababu ya kushindwa kuteua lugha ya taifa kutokana na vilugha vitumikavyo katika nchi hizo. Kwa mfano, sehemu ya kaskazini ya Ubelgiji inatumia Kiholanzi na ile ya kusini inatumia Kifaranza.

Huko Uswisi, mambo ni magumu zaidi, kwa sababu kuna lugha tatu rasmi. Kiitaliano husemwa sehemu za kusini, Kijerumani hutumiwa na wakazi wa sehemu za Kaskazini, na wale wa sehemu za magharibi husema Kifaranza.

Katika bara la Afrika, ambamo nchi nyingi zimejikomboa kutoka minyororo ya utumwa, mpaka leo hii hapajapatikana ufumbuzi wa lugha ya taifa. Ziko nchi chache sana ambazo zimelimudu jambo hili, mojawapo ni Tanzania. Hatuna budi kulionea fahari jambo hili. Ni jambo tukufu lenye kuipa heshima nchi.

Inafaa tujiulize kwa nini tatizo kama hili huzuka na kwa nini hushinda kupatiwa ufumbuzi? Sababu kubwa ni kwamba katika nchi moja huwepo vilugha au lugha nyingi ambazo hakuna moja ifaayo kuwa msingi wa kusanifisha ile ambayo itafanywa lugha ya taifa. Tatizo kama hili lilikuwepo huko Ujerumani, zama za Luther. Jambo moja lililowasaidia Wajerumani katika kusanifisha Kijerumani, ni kule kuwepo mfanano wa vilugha vyao vipatavyo vitano hivi.

Nilisema kabla kwamba tatizo la kuwa na lugha ya taifa pia lipo katika nchi zinazoendelea. Kwa mfano nchi nyingi za Afrika ya Magharibi zina tatizo hili. Nchi nyingi zimelazimika kuwa na lugha mbili au tatu maalumu katika nchi. Lugha moja huitwa lugha ya shughuli za serikali na nyingine huwa lugha ya matumizi ya kawaida kwa wananchi. Wananchi wanaweza kutumia lugha ya kabila lao kwa ufundishaji wa masomo mashuleni. Hata hivyo wanawajibika kuifundundisha lugha ya shughuli za serikali, si kwa matumizi ya kawaida bali kama somo maalum katika mfumo wao wa elimu. Hii ni kama Kiingereza au Kifaransa kilivyofunzwa wakati wa ukoloni. Utakuta pia, kwamba sehemu mbali mbali za nchi zenye uwezo wa kumudu kituo cha radio, wanatumia zaidi lugha ya sehemu ile badala ya lugha ya serikali kwa sababu wananchi wa sehemu ile wanaimudu lugha yao zaidi. Tatizo kubwa la kuzigawa sehemu za nchi moja kufuatana na lugha waisemayo, ni kwamba kunakuwa na mgawanyiko wa fikara zihusuzo utu, utamaduni na umoja wa nchi. Wananchi wanaamini wao ni wazalendo wa nchi hiyo, lakini wanajiona tofauti na wale wa sehemu nyingine ambao hawasemi lugha yao. Matatizo ya ukabila huzuka kama yalivyo katika nchi za Kenya, Uganda, Nigeria na kadhalika. Tatizo hili, kwa bahati nzuri, halipo kabisa Tanzania kwa sababu lugha ya taifa imewafanya wananchi kuimarisha umoja wao na uzalendo wao.

Nchi nyingine, ambayo imefuzu kuamua juu ya lugha ya Taifa, ni Indonesia. Wakati nchi hiyo ilipokuwa katika vita vya Uhuru, ilichagua lugha iitwayo 'Bahasa' kati ya lugha nyingine zisemwazo nchini humo. Hii ni lugha ya biashara, kama Kiswahili kilivyokuwa. Kabla ya kutangazwa kuwa lugha ya taifa, ilikuwa ikizungumzwa na watu wapatao milioni kumi. Ajabu ni kwamba lugha ambayo ilikuwa ikizungumzwa na watu wengi zaidi, yaani 'Kijava', haikuchaguliwa. Sababu kubwa iliyofanya lugha ya 'Bahasa' kuchaguliwa ni kule kuenea kwake nchi mzima. 'Kijava' kilikuwa hakikuenea nchi nzima na ingebidi watu wa sehemu nyingi kukaa chini na kuanza kujifunza. Kuenea kwake kulitokana na uenezaji wa biashara, na pia kutumika kwake katika shughuli za serikali, siasa, na uchumi. 'Bahasa' ilikuwa imetajirika kwa msamiati wake pia hasa kwa sababu ya kukopa kutoka lugha ya kwanza ya watu wa sehemu ambapo 'Bahasa' ilienea. 'Bahasa' ilikuwa na utajiri mkubwa pia wa fasihi ya lugha. Hii iliendeleza ukuaji na uenezaji wa lugha hiyo. Sababu hizi zinafanana na sababu zilizokifanya Kiswahili kuteuliwa kuwa lugha ya Taifa la Tanzania.

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu maswali haya

1. Tatizo la kuteua lugha ya taifa linaweza kutokana na nini?

2. Nchi gani ya Kiafrika imeweza kutatua tatizo la uteuzi wa lugha ya taifa? Nchi hiyo iliiteua lugha gani?
3. Je, uteuzi wa lugha ya taifa ni tatizo kwa nchi zinazoendelea tu? Thibitisha jibu lako.
4. Nchi ya Indonesia ilichagua lugha gani kuwa lugha ya taifa? Kwa nini?
5. Kutokuwa na lugha ya taifa kunaleta matatizo gani katika nchi?

Matumizi ya maneno

1. Andika neno moja lenye maana sawa na:

tatizo	ufumbuzi	hatuna budi
chache	zama	fuzu

2. Andika kinyume cha:

kushindwa	rahisi	uhuru
chache	kuwahi	kabla

Kazi Maalum

Wanafunzi wajadiliane juu ya umuhimu wa lugha ya taifa.

MSAMIATI

-bidi budi fahari fasihi fikara fuzu heshima -imarisha jirani kikamilifu -komboa kopa (ma)gumu (m)fanano (m)gawanyiko miaka nenda na miaka rudi (mi)nyororo -mudu rasmi -sanifisha sanifu/-sanifu -tajirika -tangaza -teuliwa ufumbuzi ukabila ulimwengu utu uzalendo (vi)lughu (wa)kazi wajibu -wajibika zama -zu(k)a	oblige, necessitate. obligation, necessity. fame, honor, prestige. correct, elegant, literature (English or Swahili literature). thoughts, opinion. succeed, win (as in competition or examination). honor, respect. strengthen, make firm, strengthen. neighbour. completely, precisely, accurately. liberate, rescue, redeem, free, compensate. borrow. hard, difficult. likeness, resemblance (cf. <i>fanana</i> = look alike). division, separation (cf. <i>gawanya</i> = divide.) time and time again. chain, fetters. have self control, stretch, extend oneself. official, officially. do work with skill. standard/invent, compose, standardize. become rich, wealthy. announce, declare, advertise, publicize. appointed, selected, nominated. solution. tribalism, ethnicity. universe, world. humanity, sensibility, sensitivity. patriotism, nationalism. dialects. occupants, inhabitants, dwellers. responsibility, accountability. be responsible, be accountable. (cf. <i>zamani</i>) some time in the past, period, epoch. start something, bring information out, compose.
---	--

NYONGEZA

1. Methali "Proverbs"

Waswahili hupenda sana kutumia methali katika mazungumzo yao. Kama mtu akisafiri pwani na kusikiliza wenyeji wakizungumza ataweza kuzisikia methali mbalimbali. Watoto wengi hawajifunzi methali shuleni, bali kutokana na mazungumzo ya kila siku katika sehemu wanazoishi. Siku hizi kama mtu akisafiri sehemu za Mombasa au Unguja na pemba, ataweza kuona methali zimeandikwa katika mavazi mbali mbali kama khanga au lesa. Methali hutumiwa kama njia mojawapo ya kutoa mafunzo kwa njia ya mifano. Methali moja inaweza kutoa mafunzo mbalimbali kutegemeana na uwanja wa matumizi.

Zifuatazo ni baadhi ya methali ambazo hutumiwa sana.

1. Ada ya mja hunena, 'Mungwana ni kitendo'
Public opinion maintains, 'A gentleman is judged by his actions.'
cf. Manners maketh man: or Handsome is as handsome does.
2. Aisifuye mvua imemnyea
He who praises rain has been rained on.
cf. One gives praise to something from which he has benefited.
3. Ajidhanie amesimama, aangalie asianguke.
He who thinks he has stood up, should be careful not to fall down.
cf. Once you have achieved success try to keep it up.
4. Akiba haienzi.
A reserve will not decay.
cf. Put something away for a rainy day.
4. Akili ni mali
Ability or intelligence is wealth.
i.e. If you use intelligence, you will become wealthy but if you don't use your intelligence, even if you are wealthy, it is useless because the wealth will sooner or later disappear.
5. Akili ni nywele, kila mtu ana zake
Brains are like hair, every one has his own (kind).
6. Akili nyingi huondoa maarifa.
Great wit drives away wisdom.
cf. Too clever by half.
7. Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.

- A friend in need is a friend indeed.
8. Akipenda chongo huita kengeza.
He who loves calls one eyed a squint.
cf. Love thinks no evil, Love is blind.
 9. Aliye kando haangukiwi na mti.
He who keeps to the road side will have no tree fall on him.
i.e. Do not deliberately expose yourself to danger, or get yourself involved in an unpleasant situation.
 10. Amani haipatikani ila kwa ncha ya upanga.
Peace cannot be secured save at the point of the sword.
cf. If you want peace, prepare for war.
 11. Anayekataa wengi ni mchawi.
A person who dislikes company is a wizard.
 12. Asiyefunzwa na mamaye, hufunzwa na ulimwengu.
He who was not taught by his mother will be taught by the world.
 13. Asiyekubali kushindwa si mshindani.
He who does not accept defeat is no sportsman.
 14. Asiyekujua hakuthamini.
He who does not know you does not value you.
 15. Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu.
He who does not listen to his elder's advice gets his leg broken.
i.e. By taking others advice especially our elders, one can avoid a lot of trouble.
 16. Avumaye baharini, papa, kumbe wengine wapo.
The one that is, famous in the sea is the shark, but then, there are many others. cf. Give a dog a bad name.
 17. Baada ya dhiki faraja.
After a hardship comes relief.
cf. Every cloud has a silver lining.
 18. Bendera hufuata upepo ama maji hufuata mkondo.
A flag follows the wind or water follows the current.
Used of people who keep changing sides whenever they imagine that it may be beneficial to them.
 19. Chema chajiuza, kibaya chajitembeza.
A good thing sells itself, a bad thing advertises itself for sale. cf. Good wine needs no bush.
 20. Damu nzito kuliko maji.

Blood is thicker than water.

21. *Dawa ya moto ni moto.*
The remedy for fire is fire. cf. Tit for tat.
22. *Debe shinda haliachi kutika.*
An empty cask makes most noise.
cf. He knows most who speaks least (used of people who talk a lot when they really know nothing).
23. *Dua la kuku halimpati mwewe.*
The curse of a fowl does not bother the kite (said of a situation where injustice prevails as a result of power. A powerless person can do nothing to harm a powerful person).
24. *Hakuna masika yasiyokuwa na mbu.*
There is no season of heavy rains without mosquitoes.
i.e. The troubles of one person are usually the pleasure of another.
25. *Hapana siri ya watu wawili.*
A secret is no secret when shared by two people.
cf. Three can keep a secret if two are dead.
26. *Haraka haraka haina baraka.*
Hurry hurry has no blessing. cf. More haste, less speed.
27. *Hasira hasara.*
Anger brings damage or loss.
28. *Kawia ufike.*
Better late than never.
29. *Kwa mwoga huenda kicheko na kwa shujaa huenda kilio.*
With a timid person goes laughter, with a bold person goes wailing.
i.e. Timidity often ends in a laugh, but bravado in a lament.
30. *Kidogo kidogo hujaza kibaba.*
Bit by bit, fills the bushel.
cf. Little strokes fell great oaks. Constant dripping wears away a stone.
31. *Kikulacho ki nguoni mwako.*
That which eats you up is in your clothes.
cf. It is the person who knows you well that makes trouble for you although you may not know it.
32. *Kuelekeza si kufuma na kuchumbia si kuoa.*
Aiming is not hitting or wooing is not marrying (used of people who make many plans after which they are content to sit back as though they had attained their aspiration).

33. Kukopa arusi, kulipa matanga.
Borrowing is like a wedding, repaying is like a mourning.
34. Lila na fila havitangamani.
Good and evil will not mix.
35. Lisemwalo lipo, kama halipo linakuja.
What is being talked about is there, if it is not there, it's coming along behind.
36. Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.
He who eats with you will not die for you, but he that is, born with you (will).
37. Mgema akisifiwa, tembo hulitia maji.
If the wine tapper is praised, he dilutes the palm-wine with water.
38. Mkono mtupu haulambwi.
An empty hand is not licked. cf. An empty hand is no lure for a hawk.
39. Mstahimilivu hula mbivu.
A patient man will eat ripe fruits. Patience will bring reward.
40. Mtaka cha mvunguni sharti ainame.
He who requires what is under the bed must stop for it.
There is no royal road to success (the Swahili people make use of the space under the bed for storage of utensils and other provisions).
41. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.
As you bring up a child, so will he be.
42. Mwanzo wa ngoma ni 'Lele'.
The beginning of a dance is the noise of the drum.
cf. Before a fight is a quarrel/Big things have small beginnings.
43. Ngoma ikilia sana hupasuka.
When a drum sounds loud it soon bursts (said as a precaution to people who are very ambitious).
44. Penye nia pana njia.
Where there is a will there is way.
45. Usipoziba ufa, utajenga ukuta.
If you do not fill up a crack, you will have to build a wall.
cf. A stitch in time saves nine.
46. Udongo upatize ungali maji.
Work the clay while it is still wet. cf. Strike while the iron is hot.
47. Udugu wa nazi hukutania chunguni.

The brotherhood of coconuts is a meeting in the cooking pot (said of people who do not cooperate until it is too late).

48. Ukitaka kula nguruwe, kula aliyenona.
If you want to eat pork, choose from a fat pig (Muslims are forbidden pork). cf. As well be hanged for a sheep as a lamb.
49. Wapiganapo fahali wawili, ziumiazoo ni nyasi.
When two bulls fight, it is the grass that suffers (i.e. when there is a war, the innocent suffer).

Tazama: S.S. Farsi. *Swahili Sayings. (1). 1981. Eastern Africa Publications Ltd. P.O. Box 1002 Arusha, Tanzania.* kwa methali nyingine zaidi.

2. Vitendawili "Riddles"

Vitendawili hutumiwa kama mchezo. Mtu mmoja hutega na wengine hujaribu kutegua. Kama wakishindwa, mtegaji hawezi kutoa jibu mpaka apewe kitu kizuri akitakacho kama vile mji, chombo, n.k. Kwa mfano wachezaji wanaweza kumpa mtegaji mji wa Nairobi. Akiupenda, atategua kitendawili. Asipoupenda atataka mji au kitu kingine mpaka ameridhika.

Ifuatayo ni mifano michache ya vitendawili vitumikavyo mara kwa mara.

1. Kamba yangu ndefu lakini haiwezi kufunga kuni.
2. Kipo lakini hukioni.
3. Kuku wangu katagia miibani.
4. Ninapompiga mwanangu watu hucheza.
5. Nina saa ambayo haijasimama tangu kutiwa ufunguo.
6. Mzazi ana miguu bali mzaliwa hanayo.
7. Anataga huku akitambaa.
8. Nyumba yangu kuu lakini ina mlango mdogo.
9. Nimeanika mpunga wangu juani lakini kulipopambazuka sikuuona.
10. Huku ng'o na kule ng'o.
11. Taa yangu yazagaa ulimwengu mzima.
12. Popote niendako hunifuata.
13. Haukamatiki wala haushikiki.
14. Niliona mkufu njiani lakini sikuweza kuunyakua.
15. Daima nasikia tu bali simwoni.
16. Nimemwona bi kizee amejitwika machicha.
17. Mwarabu mweupe amesimama kwa mguu mmoja.

18. Huku mwamba na kule mwamba.
19. Pana ng'ombe miongoni mwa kundi la ndama.
20. Afahamu kuchora lakini hafahamu achoracho.
21. Cheupe chavunjika manjano yatoka.
22. Hamwogopi mtu ye yote.
23. Nzi hatui juu ya damu ya simba.
24. Ni kitu gani ambacho kutoa ni kuongeza?
25. Popo mbili zavuka mto.
26. Nazi yangu yafurahisha ulimwengu pia.
27. Bwana mkubwa amelala ndani, ndevu nje zapepea.
25. Nina watoto wangu ambao daima hufukuzana lakini hawakamatani.

Majibu ya Vitendawili

- | | | |
|------------------------|--------------|----------------|
| 1. njia | 2. kisogo | 3. nanasi |
| 4. ngoma | 5. moyo | 6. kuku na yai |
| 7. boga | 8. chupa | 9. nyota |
| 10. giza | 11. mwezi | 12. kivuli |
| 13. moshi | 14. siafu | 15. upepo |
| 16. mvi | 17. uyoga | 18. kaburi |
| 19. mwezi na nyota | 20. konokono | 21. yai |
| 22. njaa | 23. moto | 24. shimo |
| 25. macho | 26. jua | 27. mahindi |
| 28. magurudumu ya gari | | |

Tazama: S.S. Farsi. *Swahili Sayings. (1). 1981. Eastern Africa Publications Ltd. P.O. Box 1002 Arusha, Tanzania.* kwa vitendawili vingine zaidi.

3. Misemo "Sayings"

Ifuatayo ni misemo michache itumiwayo mara kwa mara.

1. Anawachukua wazee wake.
He supports his parents.
2. Safari ilichukua siku nyingi.
The journey took many days.
3. Amekula chumvi nyingi.
He has lived long.
4. Nguo hizi zinakuchukua.
These clothes suit you.

5. Enda chafya.
sneeze.
6. Enda mwaya.
Yawn.
7. Piga pasi.
Iron clothes.
8. Piga mbizi.
Scuba dive.
9. Piga mluzi.
Lip whistling.
10. Piga filimbi.
Whistle using a whistle.
11. Piga kithembe.
Lisp.
12. Piga ngumi.
Punch.
13. Piga makofi.
Clap the hands.
14. Piga pembe.
Butt.
15. Piga moyo konde.
Dare, take courage.
16. Yu macho.
He is awake.
17. Kaba roho.
Throttle.
18. Futa makamasi.
Wipe the nose.
19. Vuta makamasi.
Sniff.
20. Penga makamasi.
Blow nose.
21. Enda haja.
Use the bathroom, relieve oneself in the bathroom.
22. Fanya kijicho.
Be envious, be jealous of.
23. Kaa macho.
Remain awake.
24. Katiwa notice.
Be summoned to court.
25. Andikiwa kitanda.
Be admitted in the hospital.

26. Kata tamaa.
Despair.
27. Kata shauri.
Decide.
28. Kauka sauti.
Have a hoarse voice.
29. Kunja uso.
Frown.
30. Mtu wa miraba minne.
A thick set man.
31. Kitambaa hiki kinaona.
The cloth is transparent.

MAJIBU YA MASWALI KATIKA MASOMO

Somo la kwanza

A.

- | | | | | |
|-------|-------|-------|-------|--------|
| 1. wa | 2. ya | 3. ya | 4. za | 5. la |
| 6. la | 7. wa | 8. za | 9. ya | 10. ya |

B.

1. Wafanyakazi walikuwa na furaha kwa sababu ilikuwa siku ya kupumzika.
2. Wanafunzi wana siku mbili za kupumzika kesho.
3. Walipewa nafasi ya kuzungumza na wageni.
4. Kuna mashindano mbalimbali, kama vile, mpira wa kikapu, mbio za masafa marefu, mbio za kupokezana, na mashindano ya ndondi.
5. Wanafunzi wanapenda mashindano ya mchezo wa soka.
6. Hawana maji na chakula cha kutosha.
7. Watawapa pesa na mahitaji mengine ya safari.

C.

- | | | | |
|----------------|---------|--------------|---------|
| 1. yake | 2. wake | 3. chake | 4. zake |
| 5. kwake/mwake | 6. lake | 7. wake/zake | |
| 8. yake/zake | 9. yake | 10. wake | |

Somo la Pili

A.

- | | | | |
|----------|-----------|----------|--------------|
| 1. wote | 2. wote | 3. wote | 4. wote |
| 5. chote | 6. wote | 7. kote | 8. yote/zote |
| 9. yote | 10. chote | 11. wote | 12. yote |

B.

- | | |
|-------------------|-----------------------------|
| 1. mzee ye yote | 2. ukuta wo wote |
| 3. jicho lo lote | 4. kidole cho chote |
| 5. mlima wo wote | 6. mbwa ye yote/wo wote |
| 7. mahali po pote | 8. bibi ye yote/wo wote |
| 9. shoka lo lote | 10. motokaa yo yote/zo zote |

C.

- | | | | | |
|-------|-------|-------|-------|--------|
| 1. ku | 2. ni | 3. m | 4. wa | 5. mw |
| 6. mw | 7. tu | 8. wa | 9. ku | 10. wa |

Somo la Tatu

A.

1. Mwanafunzi wa chuo kikuu cha Dar es Salaam.
2. Nyumba ya mzee Juma wa kijiji cha Mbezi.
3. Barua (wingi) za washiriki wa michezo ya Olympiki.
4. Mlangoni kwa meneja wa kiwanda cha kutengenezea viatu.
5. Kifo cha baba yake kilimsikitisha sana mama wa watoto hawa.
6. Chumbani mwa watoto kuna takataka za kila aina.
7. Meli ya Waingereza ilitia nanga katika bahari ya Hindi.
8. Uhuru wa watumwa haukapatikana mpaka Waingereza walipofika.
9. Afya za watoto hawa si nzuri ya kutosha.
10. Kusoma kwa watoto hawa hakuridhishi.

B.

mtoro	goma	kiwanda	mifuko	ndizi	ukuta
mkurugenzi	sanduku	chakula	milima	babu	ufa
mtalii	dirisha	vitanda	mzizi	simba	
wasemaji	darasa	chura		kondoo	
wazee	matunda	kijito		mbuzi	
	somo	vitoto			
	majia	vijembe			
	mabuzi				
	rafiki				
	embe				
	buzi				
	madege				
	majitu				
	marafiki				
	mababu				

pahali
mahali

C.

- | | | | |
|----|----------------|----|----------|
| 1. | vizuri, vibaya | 2. | vigumu |
| 3. | vikali | 4. | polepole |
| 5. | upes | 6. | taratibu |
| 7. | haraka. | | |

Somo la Nne

A.

- | | | | | | | | |
|----|-----|-----|---|----|------|----|----|
| 1. | vyo | 2. | o | 3. | kapo | 4. | zo |
| 5. | o | 6. | o | 7. | kazo | 8. | yo |
| 9. | yo | 10. | o | | | | |

B.

1. Vyombo ambavyo alinunua havifai kutumiwa katika nchi za joto.
2. Uhuru ambao anazungumzia ni uhuru wa bendera.
3. Mahali ambapo tutafanyia sherehe ni hapa.
4. Mila na desturi ambazo mlitaja ni za nchi gani?
5. Panya ambao wanawasumbua wakulima huanza kutokea baada ya masika.
6. Aliwaleta wageni ambao walifika jana.
7. Tuletee motokaa ambazo zitaweza kupanda milima hii bila matatizo.
8. Wanakunywa maziwa ambayo yalioza.
9. Milima hii ni ile ambayo tulisikia kwamba ina madini za kila aina.
10. Walitumia wanyama ambao waliletwa kutoka bara kwa shughuli za utafiti katika maabara yao.

C.

1. Vyombo ambavyo hakununua havifai kutumiwa katika nchi za joto.
2. Uhuru asiozungumzia ni uhuru wa bendera.
3. Mahali ambapo hatutafanyia sherehe ni hapa.
- 3b. Mahali tusipofanyia sherehe ni hapa.
4. Mila na desturi ambazo hamkutaja ni za nchi gani?
5. Panya wasiowasumbua wakulima huanza kutokea baada ya masika.
6. Aliwaleta wageni ambao hawakufika jana.
7. Tuletee motokaa ambazo hazitaweza kupanda milima hii bila matatizo.
- 7b. Tuletee motokaa zisizoweza kupanda milima hii bila matatizo.
8. Wanakunywa maziwa ambayo hayakuoza.
9. Milima hii ni ile ambayo hatukusikia kwamba ina madini za kila aina.

10. Walitumia wanyama ambao hawakuletwa kutoka bara kwa shughuli za utafiti katika maabara yao.

Somo la Tano

A.

1. Mwanamke alikwenda dukani kutunulia mahitaji yetu.
2. Huyu ni ng'ombe wa nani?
3. Maneno niliyokuambia ni ya kweli kabisa.
4. Ng'ombe wetu amepotea.
5. Mimi nilimwambia alale vizuri.
6. Vifo vimezidi katika mji wetu/miji yetu.
7. Mti huu hauwezi kuanguka.
8. Nilikwenda Nairobi kwa sababu ya kuwaona wazazi.
9. Wachezaji wa mpira wa miguu wako hapa.
10. Wavuvi walipumzika karibu na bahari.

B.

1. Chai ya asubuhi watapikiwa watoto.
au
- 1b. Chai ya asubuhi itapikiwa watoto.
2. Mwalimu aliendewa nao ofisini.
3. Habari zote zitasemwa naye.
4. Chupa tatu za bia zitanywiwa nawe
5. Kiingereza huzungumzwa na watu wa sehemu nyingi za dunia.
6. Pesa zote zitachukuliwa naye atakapofika.
7. Atafungwa (naye) kamba miguuni.
8. Mtoto mzuri alizaliwa na mama hospitalini.
9. Kesi iliamuliwa na jaji bila shida.
10. Motokaa yake ilitengenezwa nao lakini bado ni mbovu.

Somo la Sita

A.

- | | | | |
|------------|------------|------------|-------------|
